

**Kiwanda** cha kusarifu dagaa kuinua uchumi wa Zanzibar UK. 17



**Wapinzani** Kongo kuandamana kupinga uchaguzi UKURASA 19





UONGOZI NA WAFANYAKAZI WA NIPASHE, UNAWATAKIA HERI YA SIKUKUU YA KRISMASI



# Nipashe

**Jumatatu Desemba 25, 2023** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581535

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


SIMULIZI:

# Mama alivyookoa watoto 11 maporomoko Hanang’

UKURASA 2



Paula Neema akizungumza na mwandishi wa habari wa gazeti hili kwenye makazi ya muda anayoishi katika Shule ya Msingi Genana. Pembeni ni nyumba aliyokuwa anaishi katika Kijiji cha Gendabi na familia yake. **PICHA: MOHAB DOMINICK**

UKURASA WA 3

## MAKONDA: VIONGOZI WA DINI LIOMBEENI TAIFA, RAIS SAMIA

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, ametoa wito kwa viongozi wa dini nchini...



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, akiombewa na Askofu wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Dar es Salaam, Askofu Jackson Sosthenes, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

RIPOTI MAALUM

## Kutoka neema hadi kubahatisha

UKURASA 4

## Ajali ilivyoua wanane Kibondo

UKURASA 2


**MICHEZO** GAMONDI AKUBALI MUZIKI TABORA UTD UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




# Simulizi ya mama aliyeokoa watoto 11 maporomoko ya tope Hanang'

**Na Mohab Dominick,** HANANG'

"...NILIKIONA kifo kabisa, lakini ukuu wa Mungu unabaki kuwa ukuu wake. Hayo maporomoko yalipita nyuma ya nyumba yangu nikiyaona nikiwa na wanangu lakini huwezi amini nilipata ujasiri wa kuwaongoza."

Ni manusura wa maporomoko ya tope, mawe na magogo kutoka Mlima Hanang, mkoani Manyara na kuua watu 89, kujeruhi 116, Paula Neema, akisimulia kilichotokea siku hiyo akiwa na watoto wake 11 ndani ya nyumba.

Anasema anaona ni kama ndoto yeye na familia yake ya watoto hao kuwa wazima hadi sasa. Maafa hayo yalitokea usiku wa Desemba 3, mwaka huu, baada ya mlima huo uliokuwa umenyonya maji mengi yaliyotokana na mvua kubwa kumeguka na kuanza kuporomosha tope zito na magogo kwenye nyumba zilizopo karibu.

Paula Mkazi wa Kijiji cha Gendabi, alisema wakati wa tukio hilo Mungu alimpa nguvu na ujasiri wa kuiokoa familia yake na kufanikiwa kuwakimbiza kuelekea eneo la uwanda wa juu wa Shule ya Msingi Gendabi.

"Nilikiona kifo kabisa, lakini ukuu wa Mungu unabaki kuwa ukuu wake. Hayo maporomoko yalipita nyuma ya nyumba yangu nikiyaona nikiwa na wanangu, lakini huwezi amini nilipata ujasiri wa kuwaongoza kukimbilia eneo la milimani na wakati huo sikukumbuka mifugo yangu, hasa ng'ombe.

Neema anasema kuwa baada ya maji kupungua alirudi nyumbani kwake na hakukuta chochote ikiwamo mifugo hiyo ambayo alikuwa akifuga.

"Kwa sasa maisha yanaendelea kama kawaida nikiwa na ujauzito wa mtoto wa 12, lakini inapofika majira ya saa 12 za jioni mimi na familia yangu tunarudi katika hifadhi ambayo ipo katika Shule ya Msingi Gendabi katika Halmashauri hiyo ya Hanang."

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama, uchunguzi wa kijiolojia uliofanywa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) katika tukio hilo hakukuwa na tetemeko la ardhi, wala mlipuko wa volcano katika Mlima Hanang'.

Mhagama alinukuliwa akisema; "Miamba hiyo ilinyonya maji ya mvua na kuporomoka, na hivyo kutengeneza tope kubwa na kipande hicho kilichomeguka kilinyonya maji na kusababisha mgandamizo na sehemu ya mlima, ikashindwa kuhimili mgandamizo huo na hivyo kutengeneza tope lililoanza kuporomoka kwa kasi na kutengeneza njia kufuata mkondo wa Mto Jorodom."

Maeneo yaliyoathirika zaidi na maafa hayo ni Mji Mdogo wa Katesh na kata zake, ambazo ni Jorodom na vitongoji vyake vya Udameseki, Gawal na Jorodomu Kati.

Pia zimo Kata ya Gadang'a na vitongoji vyake vya Gadang'a A, Gadang'a B, lakini Kata ya Katesh A na Gedang'ongyi na Kata ya Katesh, vitongoji vya Kates Stendi na Katesh B.

Aidha, zimo pia Kata ya Gendabi, Kijiji cha Gendabi katika vitongoji vya Uhuru na Dumanang'.

Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni Gendabi, Samson Israel, alimwomba Rais, Samia Suluhu Hassan, kuona uwezekano wa kuwahamisha katika eneo hilo, kwa kuwa kwa sasa halifai kuishi binadamu.

### MISAADA YAMIMINIKA

Jana Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alieleza kuwa serikali imeendelea kupokea na kugawa misaada ya chakula na mahitaji muhimu kwa waathirika wa maafa ya Hanang' mkoani Manyara.

Alisema hadi kufikia jana misaada ya chakula na mahitaji muhimu imefikia thamani ya Sh. bilioni 2.5 na fedha taslimu Sh.bilioni 5.2.

Alisema fedha taslimu zinajumuisha shilingi bilioni 2.5 zilizoletwa na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Sh.bilioni 2.7 zilizomo kwenye akaunti ya Mfuko wa Taifa wa Misaada ya Maafa inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 2.2 zimechangwa na taasisi na mashirika ya umma kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina na Sh. milioni 419.4 zimechangwa na wahisani mbalimbali.

Matinyi alisema: "Wakati serikali ikiwashukuru Watanzania kwa utu, upendo, uzalendo na moyo wa kujitolea ambao umesaidia kupatikana kwa chakula cha kutosha na mahitaji muhimu ili kuwasaidia waathirika kuendelea na maisha yao, inatoa wito pia kwa wanaoendelea kuleta misaada kujikita zaidi katika vifaa vya ujenzi."

### KAMBI ZAFUNGWA

Matinyi alisema serikali ilianza kugawa chakula na mahitaji mengine muhimu kwa waathirika kwenye kambi tatu, huku ikiwasaidia kuungana na ndugu zao.

Alisema kambi hizo tatu sasa zimefungwa baada ya waathirika wote 690 kutoka kaya 140 kurejea makwao na kwa ndugu zao. Matinyi alisema waathirika 534 walikuwa wakilala kambini na 156 walikuwa wakija asubuhi na kuondoka jioni.

### UGAWAJI MISAADA

Alisema mgawo wa misaada unalenga kwanza waathirika 1,292 waliothibitika kupoteza nyumba zao ama kuharibika au kuingia tope.

Matinyi alisema idadi hiyo ilipatikana baada ya tathmini ya kina ya picha za satelaiti, rekodi za sensa, ukaguzi halisi wa nyumba hadi nyumba na rekodi za serikali za mitaa katika ngazi ya vitongoji, vijiji na kata.

Alisema utaratibu wa ugawaji misaada uliwekwa kwa kubandika majina ya waathirika kwenye ofisi za kata baada ya kukamilika kwa tathmini ambapo mhusika akifika huelekezwa kituo chake cha kupokelea misaada.

Matinyi alisema tangu wiki iliyopita wananchi wamekuwa na ratiba za kwenda kupokea misaada kila siku kutokana na wingi wa misaada hiyo.

"Kwa wastani kila kaya inapata chakula cha kutosha miezi sita au zaidi ambapo kwa baadhi ya bidhaa kama sukari wananchi hao wanapewa ya kutosha kutumia kwa zaidi ya miaka miwili kwa mujibu wa vipimo vya lishe," alisema.

Matinyi alitaja misaada inayotolewa ni chakula cha mahindi, ngano, mchele, unga wa mahindi, unga wa ngano, maharage, mafuta ya kula, maziwa, unga wa lishe kwa watoto, mayai, sabuni, magodoro, mablanketi, mashuka.

Vingine ni mikeka, ndoo, majiko ya kupikia ya gesi na mitungi yake, masufuria, nguo, viatu, kandambili na vingine vingi.

### WALIOFARIKI, MAJERUHI

Matinyi alisema idadi ya watu waliopoteza maisha hadi sasa ni 89 tangu Desemba 11 na mwili mmoja wa mtoto wa kike bado haujatambuliwa.

Aalisema hadi sasa majeruhi wanne bado wanatibiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara iliyopo mjini Babati na mmoja amepelekwa Hospitali ya Benjamin Mkapa jijini Dodoma, kwamba serikali imegharamia matibabu, mazishi na kutoa mkono wa pole kwa wafiwa, majeruhi walikuwa 139.

# Ajali ilivyoua wanane Kibondo

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

WATU wanane wamefariki dunia na wengine sita kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha magari mawili katika Barabara ya Kibondo-Kakonko, Kijiji cha Mumkugwa, Wilaya ya Kibondo, mkoani Kigoma.

Ajali hiyo ilihusisha gari yenye namba za usajili T833 DUA aina ya FAW mali ya kampuni ya CHICCO na gari ndogo aina ya Toyota Probox yenye namba za usajili T 890 DYZ.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Mkoa Kigoma, Thobias Andengenye, alisema imetokea juzi saa 11 jioni ikihusisha gari hiyo ndogo iliyokuwa ikifanya safari zake kati ya Kibondo na Kakonko.

Andengenye alisema kuwa hadi kufikia jana asubuhi miili ya watu sita ilikuwa imetambuliwa na kuchukuliwa na ndugu zao na miili ya watu wawili bado ipo katika Hospitali ya Wilaya Kibondo na kuwasisitiza watu kufika hospitalini hapo kuitambua.

Aliwataja waliofariki kwenye ajali hiyo kuwa ni dereva wa gari ndogo, Hamisi Chaurembo (27), Bernadina Reuben (22), Madua Asukile, Ntiganiza Bihezako (67), Vedastus Paul (28), Vladmir Vedastus (1) na marehemu wengine wawili ambao majina yao hayajatambuliwa hadi sasa.

Alisema kati ya majeruhi sita, watatu wametibiwa na kuruhusiwa kurudi nyumbani na watatu waliobaki wameonekana kuhitaji matibabu zaidi na watahamishiwa Hospitali ya Rufani ya Bugando, Mwanza.

Aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni dereva wa gari la CHICCO, Flavian Felishian (28) aliyejeruhiwa kichwani na kifuani, Juma Saidi (27), Daniel Samwel (33), Silvanus Muhigwa (43) Sara Bundala na Dori Mafumbo (22).

Mkuu wa mkoa alitoa pole kwa ndugu wa marehemu na kusisitiza wakazi wa mkoani humo kuchukua tahadhari barabarani hasa wakati huu wa likizo ya mwisho wa mwaka kunakuwa na ongezeko kubwa la vyombo vya usafiri barabarani.

"Nitoe wito kwa watumiaji wa vyombo vya moto, wahakikishe wanachukua tahadhari wanapokuwa barabarani kwa kipindi hiki cha msimu wa sikukuu ili kupunguza au kutokomeza ajali," alisema Andengenye.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Filemon Maungu, alisema uchunguzi wa polisi umebaini kuwa chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi na uzembe wa dereva wa gari ndogo ambaye alishindwa kulimudu gari hilo kwenye kona kali na kugongana uso kwa uso na gari hilo la CHICCO.

HABARI KITAIFA

# Kila kaya kupanda miche 10 ya parachichi Njombe

**Na Mwandishi Wetu,**
NJOMBE

MKOA wa Njombe umejipanga katika miaka mitano ijayo kila kaya iwe na uwezo wa kuzalisha matunda ya parachichi yatakayowaingizia kipato kisichopungua Shilingi milioni mbili kila wanapovuna matunda hayo.

Mratibu wa Uchumi wa Mkoa wa Njombe, Musa Selemani, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa wahariri wa vyombo vya habari walioenda mkoani humo kwenye ziara ya kikao kazi cha utekelezaji wa awamu ya tatu ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III).

Selemani alisema katika jitihada za kuendelea kuzijengea uwezo wa kujitegemea kaya za wanufaika wa TASAF III, mkoa huo umeanzisha mradi maalumu wa kilimo cha parachichi ambao kila kaya yenye eneo na itakayoridhia itawezeshwa angalau miche 10 ya kuanzia.

Akifanunua kuhusu kilimo hicho, Selemani alisema katika miche 10 inatarajiwa kila mmoja kutoa matunda 200 ambayo kilo moja itauzwa Sh. 1,000.

"Ifikapo miaka mitatu tangu kupandwa kila mche una uwezo wa kuzalisha kilo 400 za matunda utakapofikisha miaka mitano ikiwa utatunzwa kama inavyotakiwa," alisema.

Alisema mkoa huo umezindua mradi huo mwezi Januari, mwaka huu na utekelezaji unafanyika kwa awamu kwa kaya zote 24,874 za wanufaika ndani ya mkoa.

Selemani alisema awamu ya kwanza ya utekelezaji imeanza na kaya zote 1,804 zilizokidhi vigezo (utayari na kuwa na eneo la kudumu) katika Halmashauri ya Mji wa Makambo, zimewezeshwa kati ya mche mmoja hadi 20 na zinaendelea kujifunza kwenye mashamba yao chini ya wataalamu wa kilimo tangu Machi. 2023.b"Maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo katika halmashauri zilizosalia yanaendelea na utekelezaji unatarajiwa kufanyika mwezi Machi, mwakani," alisema.

Mratibu wa TASAF Njombe, Kelvin Kapungu, alisema kutokana na mradi huo wa zao la parachichi, wanufaika wamehamasika na kuamua fedha zao kukatwa kwenye dirisha ili ziwawezeshe kununua miche na kupanda kwenye maeneo yao.

Kapungu alisema, mradi wa kilimo cha parachichi utawasaidia walengwa hata mpango wa TASAF utakapoisha watakuwa na uwezo wa kusimama wenyewe bila kutegemea fedha za mpango.

Bwana Shamba Salivius Kawogo, aliwaambia wahariri kuwa jukumu analolifanya ni kuwashauri walengwa kufuata kanuni za upandaji na utunzaji miti ili waweze kupata mavuno bora.



Mratibu wa Uchumi wa Mkoa wa Njombe, Musa Selemani, akiongea na Wahariri.

# Makonda: Viongozi wa dini liombeeni taifa, Rais Samia

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, ametoa wito kwa viongozi wa dini nchini kuendelea kuiombea Tanzania na Rais Samia Suluhu Hassan katika majukumu yake ya kuwatumikia wananchi.

Alitoa wito huo jana alipomtembelea Askofu wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Dar es Salaam, Jackson Sosthenes, ikiwa ni mwendelezo wa ziara zake za kuwatembelea viongozi na watu wa makundi mbalimbali katika jamii, lengo kuu likiwa ni kuendeleza ushirikiano na kupokea ushauri.

Alisema ni vizuri viongozi wa dini kuendelea na moyo wa imani wa kuiweka nchi katika maombi pamoja na kumuombea Rais Samia.

Makonda alisema viongozi hao wa kiroho katika jamii wanapaswa kuendelea kuenzi utamaduni mzuri wa siku zote wa dini na madhehebu mbalimbali kushirikiana na serikali.

Alisema utamaduni huo ambao ulianza tangu awamu ya kwanza hadi serikali ya sasa ni vizuri ukaendelea kuenziwa kwa maslahi mapana ya nchi.

Askofu Sosthenes alisema wataendelea kuliombea Taifa na Rais Samia ili azidi kuwa imara katika kazi anayoifanya ya kuwaongoza Watanzania.

Aidha, alimtakia kila la kheri Makonda katika utendaji wa majukumu yake, hasa anaposhiriki katika maamuzi mbalimbali ya kusaidia chama, serikali na nchi kwa ujumla.

"Lakini zaidi sana Mungu akamuongoze Rais wetu Samia Suluhu Hassan usiku na mchana, awe na moyo mkuu katika kuongoza Tanzania na kuwaongoza watu wake na kuwafikisha mahali ambapo wewe Mungu umekusudia,"



Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, akiombewa na Askofu wa Kanisa la Anglikana, Dayosisi ya Dar es Salaam, Askofu Jackson Sosthenes jana. **NA MPIGAPICHA WETU**



KUTOKA NEEMA HADI KUBAHATISHA...

# Matajiri wa samaki waambulia patupu ziwani

**Na Sanula Athanas aliyekuwa**
UKEREWE

UMAARUFU wa Ukerewe ulibatizwa jina la "Kisiwa cha Samaki". Leo hii si jina la kutamkwa tena, au kutamkwa kwa kigugumizi.

Mvuvi aliyekuwa anarejea kutoka kazini akiwa na kilo 200 za samaki, sasa anaambulia kilo 20; wafanyabiashara walionunua tani tatu za samaki na kuziingiza sokoni, hesabu yao ya sasa ni kilo 250.

Hayo yanajitokeza huku kukiwa na lingine la kimazingira; maji ya Ziwa Victoria yameshasogelea makazi na kumeza baadhi ya nyumba, vibanda vya biashara na mashamba.

Soko lao la Kakukuru, soko kubwa zaidi la samaki wilayani Ukerewe, nalo liko kwenye 'baibai', limeshabomolewa na maji upande mmoja.

Katika kujihami kwa hali ya sasa, licha ya hatari iliyopo, soko hilo linatumika 'hivyohivyo' kupokea, kupima na kuuza samaki.

Kilio cha ugumu wa maisha kwa wakazi kinazidi kuwa msamiati wa kawaida kisiwani Ukerewe. Majumuisho ya yote ni kwamba ufukara unawanyemelea kama si kuwafikia tayari.

Mvuvi Clifford Costantine, mkazi wa Kakukuru, anasimulia namna ulivyo mtihani mgumu kwao kupata samaki ziwani.

"Zamani ilikuwa kawaida tu kurejea na kilo 200, lakini sasa tunaambulia kilo 50 hata kilo 20 tu wakati mwingine. Upatikanaji wa samaki umekuwa mgumu mno.

"Tunashindwa kuelewa sababu ni nini hasa. Wataalamu wa halmashauri wanatuambia ni athari za mabadiliko ya tabianchi. Kila tunakokwenda (kuvua) tunakosa samaki.

"Kwa sasa tunavua Ukara na Uvinza, huko walau tunaambulia chochote. Kwa maeneo yetu haya ya karibu, kuna shida kubwa. Samaki hawapatikani," anasema.

Ni kilio kinachosikika pia kwa mvuvi Varency Vamiji, anayesema kuwa kutokana na samaki kuadimika Ukerewe na maeneo jirani, wanalazimika kuvuka mpaka hadi Uganda, wanakokumbana na misukosuko mbalimbali ikiwamo kunyang'anywa samaki na askari wa nchi hiyo wanaofanya doria ziwani.

Mvuvi Neema Mashimba ni mkazi wa kitongoji cha Makutano, kijijini Muritilima, Kata ya Kakukuru. Licha ya kumiliki mitumbwi miwili ya uvuvi, analalama maisha yao yamekuwa magumu kutokana na uhaba wa samaki ziwani.

"Kwa kweli tumeathirika sana, maisha yetu yamekuwa magumu. Zamani nilikuwa na uhakika wa kupata kilo 50 (za samaki) kwa siku, lakini sasa ninaambulia kilo tano, ni hasara tu!



Soko la Samaki Kakukuru wilayani Ukerewe likiwa limebomolewa na maji ya Ziwa Victoria. **PICHA: SANULA ATHANAS**

"Kausha damu (mikopo yenye masharti magumu ya marejesho) zimekuwa nyingi. Soko letu (la Kakukuru) nalo kama unavyoona limeharibika. Usalama wetu hapa sokoni ni mdogo. Watu wengi hawana imani tena na soko hili.

"Nina miaka mitano ninavua hapa Kakukuru na visiwa jirani. Nilianza na mtaji wa Sh. milioni tatu. Uchumi wangu unategemea samaki," anasema Neema, mama wa watoto wawili anayejivunia kujenga nyumba na kununua gari kupitia shughuli za uvuvi na biashara ya samaki kisiwani Ukerewe.

Mzee Yusuph, mfanyabiashara wa samaki na mkazi wa Kakukuru, anasema wameathirika kutokana na uhaba wa samaki, hali kadhalika Soko la Kakukuru kufikiwa na maji ya ziwa yaliyosogelea makazi yao.

Anasema wavuvi wengi wameamua kuachana na soko hilo na kusababisha anachokiita "ukata wa samaki sokoni".

"Lijengwe soko lingine mbali na maji ili tupate samaki. Tulikuwa tunapata tani mbili hadi tatu hapa sokoni kwa siku. Lakini kwa sasa huwezi kupata samaki wa kiasi hicho.

"Tunaambulia kilo 250 kwa siku. Hatuwezi kumudu kuendesha maisha yetu tena," analalama mfanyabiashara huyo.

Richard Msafiri, Mwenyekiti wa Kijiji cha Masonga, Kata ya Kakukuru, anasema ugumu wa kuwapata samaki, umesababisha changamoto za kiuchumi na kijamii, zikijumuisha baadhi ya wavuvi wenzake kutelekeza familia.

"Kukishakuwa na ugumu wa kupata samaki katika maeneo yetu haya ya Ukerewe, sisi wavuvi inabidi tusafiri kwenda visiwa vya mbali na kuziacha familia zetu.

"Huko kambini mvuvi akishakaa siku nyingi na anakula na kushiba, anatafuta mama mwingine huko. Hapo sasa panaibuka matatizo mengine ya kupata magonjwa na zinaa na kusababisha mimba. Akirejea huku Ukerewe, anatelekeza hiyo familia yake mpya ya kambini.

"Kule kisiwa cha Godzba ni kawaida tu kukuta kichanga kimetupwa. Na kuna kinamama wengi tu huku visiwani wana watoto ambao baba zao hatuwajui. Anayebaki na mzigo ni mama, ndiye mwenye jukumu la kulea.

"Mwaka 1994 hapa kijijini (Masonga) waliweka kambi wavuvi kutoka Kigoma, walikuja kwa wingi. Tuliona matokeo yake, mpaka leo tuna vijana ambao ni matokeo ya kambi hiyo. Wavuvi waliwapa mimba mabinti wa hapa, kisha wakaondoka, wakarejea makwao.

"Huku visiwani tunajuana 'fulani ni matokeo ya kitu hiki, fulani ni matokeo ya kambi fulani ya wavuvi'. Elimu kwa wananchi inatolewa ili kuepuka kuwa na watoto wanaolelewa na mzazi mmoja," Mwenyekiti Msafiri anasema.

Mkusanyaushuru katika Soko la Kakukuru, Josephat Pembogoto, anakiri hali ya mapato sokoni si nzuri, akiwa na ufafanuzi:

"Mwanzoni hali ilikuwa nzuri sana, ilikuwa kawaida tu hapa sokoni kukusanya ushuru wa hadi Sh. 200,000 kwa siku, lakini sasa samaki hawapatikani kwa wingi. Kuna siku tunajikuta tumeambulia Sh. 50,000 tu," anasema.

Anafafanua kuwa mapato hayo yanatokana na ushuru unaotozwa na halmashauri kwa wavuvi; Sh. 100 kwa kila kilo ya dagaa na Sh. 300 kwa kila kilo ya samaki (mfano sangara na sato).

Pembogoto anasema kuwa mbali na ugumu wa kuwapata samaki ziwani, kubomolewa kwa soko lao pia kumeathiri mapato. Wavuvi wanahofia usalama wao sokoni.

Akiwa katika Soko la Kakukuru mnamo tarehe 8 ya mwezi uliopita, mwandishi aliona dalili za soko hilo kuporomoka wakati wowote; upande wa magharibi tayari umeshabomolewa na maji, kuna nyufa katika kuta, na msingi wake umeshachimbuliwa na maji ya ziwa yanayokupwa na kujaa.

Fabian Mtaki, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Muritilima liliko Soko la Samaki Kakukuru, anasema lilijengwa mwaka 2010 kwa gharama ya Sh. milioni 14.

Anarejea historia ya mradi huo, akisema soko lilijengwa mbali na mwalo, lakini kutokana na mvua kubwa iliyonyesha miaka ya 2000 na 2021, eneo hilo limefikiwa na maji ya ziwa. Mchakato wa kujenga soko jipya unaendelea.

Diwani wa Kakukuru, Moses William, anasema hoja ya ujenzi wa soko jipya wameshaiwasilisha katika vikao vya Baraza la Madiwani. Wameshauri kujengwe soko la kisasa mbali na maji.

William pia anasema wameshirikiana na wataalamu wa halmashauri kutoa elimu kwa wananchi, wakiwataka waache kujenga nyumba na kuendesha shughuli za kilimo karibu na mwalo.

Anasema elimu hiyo inatolewa kwa wananchi kwa kuzingatia angalizo lenye ushuhuda wa kilichojiri katika vijiji vya Muritilima na Masonga ambako soko la samaki, nyumba, mashamba, miti na vibanda vya biashara vimemezwa na maji ya ziwa kutokana na mvua kubwa ya mwaka 2021.

Ofisa Mapato wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Longino Ondole, anasema kinachowasibu wavuvi, kimeathiri pia mapato ya halmashauri. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, waliweka lengo la kukusanya Sh. bilioni 1.795, lakini walikusanya Sh. milioni 903.616, sawa na asilimia 50 ya makadirio yao.

Katika hilo, Ofisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Justine Nazi, ana ufafanuzi wa ziada. Anasema kilichoshuhudiwa mwaka 2021 na kinachojiri sasa Ukerewe ni matokeo ya mvua kubwa iliyonyesha mwishoni mwa mwaka 2020 na mwanzoni mwa mwaka 2021.

"Mabadiliko ya tabianchi yametuathiri sana katika sekta ya uvuvi hapa Ukerewe. Upatikanaji wa samaki na mazao yake umekuwa mgumu. Ikumbukwe kwamba uchumi wa Ukerewe unategemea samaki kwa asilimia 85.

"Mvua kubwa iliponyesha, ilisababisha mafuriko ambayo yaliharibu mazalia ya samaki, hivyo kuathirika uzalianaji wa samaki," anafafanua.

Hassan Bomboko, Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, anasema mabadiliko ya tabianchi yameathiri sekta ya uvuvi wilayani mwake kutokana na kuwa chanzo cha kuharibu mazalia ya samaki.

'Mabadiliko ya tabianchi pia yamesababisha kipato cha wananchi wetu kupungua kwa sababu samaki hawapatikani kwa urahisi. Tuna maeneo ambako maji ya ziwa yamevamia, mfano kule Ghana, Kamasi na Bwiro.

"Tumejitahidi kuwaelimisha wananchi waepuke kujenga makazi karibu na ziwa na madhara yanayoweza kutokea," anasema.

## UTAFITI LHRC

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) hakiko mbali na yanayoendelea Ukerewe. Katika ripoti yake ya Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwenye Haki za Binadamu, Uchumi na Mazingira Tanzania kiliyoitoa Machi mwaka huu, kituo hicho kinabainisha kuwa athari za mabadiliko hayo zinajumuisha kuharibiwa mazalia ya samaki kulikosababisha kupungua kwa samaki.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, anasema wavuvi, wakiwamo wa Ukerewe, wameathirika kutokana na kuwapo vipindi vya upepo na dhoruba vinavyofanya uvuvi kuwa shughuli hatari, pia kupunguza lishe na mapato kwa maelfu ya wenyeji wanaotegemea ziwa kupata chakula na mapato.

## KUHUSU UKEREWE

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya Bomboko, Wilaya ya Ukerewe inaundwa na visiwa 38 (15 vinakaliwa na watu), tarafa nne, kata 25, vijiji 76 na vitongoji 513. Ina wakazi 387,817 (Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022).

# Salamu za Krismasi na Mwaka Mpya

Na Balozi Dk. Michael Battle




Balozi Dk. Michael Battle

MKE wangu Linda na mimi, tuliwasili Tanzania kwa furaha mwanzoni mwa mwaka 2023 ili kuanza ngwe yangu ya pili nikiwa na wadhifa wa balozi.

Toka wakati nilipokabidhi nyaraka zangu za utambulisho kwa Rais Samia Hassan, nimejitoa kwa dhati kushirikiana na Serikali ya Tanzania kuendelea kuimarisha ushirikiano wetu rasmi ili kuimarisha amani, ustawi, usalama na afya kwa raia wote.

Tunaadhimisha kipindi cha sikukuu pamoja na familia na wapendwa wetu, ningependa kuchukua fursa hii kurejea na kutafakari yale tuliyoweza kuyafanikisha pamoja, wakati tukijiandaa kwa kazi iliyo mbele yetu mwaka 2024.

Kuongeza biashara na uwekezaji kati ya Marekani na Tanzania ni mojawapo ya mambo ninayoyapa kipaumbele cha juu nikiwa Balozi.

Kufuatia mkutano wa Kihistoria kati ya Rais Samia na Makamu wa Rais Kamala Harris mwanzoni mwa mwaka, tulijizatiti na kukamilisha majadilino ya kibiashara (Commercial Dialogue) na wenzetu Watanzania.

Majadiliano ni ahadi na azma ya serikali zetu kuboresha biashara na uwekezaji wa pande zote mbili, kuboresha mazingira ya kufanya biashara kupitia teknolojia, uwazi na mageuzi ya kikanuni na kisheria.

Majadiliano ya Kibiashara yatakwenda sambamba na mkakati wa kukuza uchumi wa USAID.

Ninaposafiri katika nchi hii nzuri kutoka Zanzibar hadi Kigoma au Arusha hadi Mbeya, ninakutana na wawakilishi wa serikali, viongozi wa asasi za kiraia, wahitimu na washiriki wa programu zetu mbalimbali na wawakilishi wa sekta binafsi nikilenga katika kukuza fursa za kibiashara kwa Wamarekani kufanya kazi na Watanzania.

Chukulia kwa mfano, kitengo cha Kilimo cha USAID, ambacho katika mwaka 2023 kilitenga zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 30 kwa maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa na Serikali ya Tanzania.

Hii ni pamoja na kuweka msingi wa kujenga kitovu cha uzalishaji mbolea, kuongeza tija na uzalishaji wa kilimo, kukuza teknolojia za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi na kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo.

Msaada huu umeandaliwa mahsusi kuongeza biashara na uwekezaji ukienda sambamba na malengo ya Mkutano wa Kilele wa Viongozi wa Marekani na Afrika.

Zaidi ya hayo, USAID imeboresha uhifadhi wa takriban hekta milioni mbili za ardhi huku ikiwasaidia watu 64,000 kuongeza kipato chao kupitia uhifadhi wa hazina kubwa ya maliasili za Tanzania. Kukiwa na ongezeko kubwa la watalii na wanafunzi wa kigeni wanaokuja Tanzania, ninafahamu kwamba mambo mazuri bado yanakuja mbele yetu.

Usalama wa Afya kimataifa bado unaendelea kuwa eneo muhimu katika ushirikiano wetu, na uwekezaji mkubwa zaidi wa Marekani unalenga kusaidia afya ya raia wa Tanzania.

Tangu mwaka 2003, PEPFAR imetoa Dola za Kimarekani bilioni saba kwa ajili ya kusaidia kinga, huduma na matibabu ya VVU, na kuimarisha mfumo wa afya nchini Tanzania. Kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, PEPFAR kwa sasa inawasaidia zaidi ya watu 1.4 milioni wanaoishi na VVU kwa kupata na kutumia dawa za kufubaza VVU.

Katika Siku ya Ukimwi Duniani, nilifurahi kuona Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitangaza matokeo ya Utafiti wa Athari za VVU nchini Tanzania wa mwaka 2022 - 2023, ukionyesha kwa Tanzania iko karibu kudhibiti janga la VVU.

Waziri Mkuu alikuwa sahihi alipotoa wito kwa vijana na wanaume kwenda kupima VVU. Tanzania iko karibu sana kufikia malengo ya UNAIDS ya 95-95-95, na upimaji wa VVU ndio ufunguo wa kufikia lengo hilo.

Pale ugonjwa wa Marburg ulipogundulika kwa mara ya kwanza nchini Tanzania mwezi Machi, sekta ya afya iliwasiliana na washirika wa kimataifa na kushughulikia changamoto hiyo kwa uwajibikaji na uwazi mkubwa. Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Maradhi cha Marekani (CDC) kwa fahari kubwa kilishirikiana na Serikali ya Tanzania ili kusaidia katika ufuatiliaji, epidiemolojia na usimamizi wa data ili kudhibiti mlipuko, ambao ulitangazwa rasmi kuwa umekwisha tarehe 2 Juni 2023.

Nikiwa Balozi, nimefurahishwa sana na falsafa ya Rais kuwa nguzo za demokrasia za vyama vingi nchini Tanzania kuwa ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Ujenzi Mpya, na ninawahimiza timu yetu ya ubalozi kufanya kazi kwa kuzingatia falsafa hii kuitia moyo Tanzania ichukue hatua muhimu, stahiki na zenye maana kuelekea mageuzi ya kweli ya kidemokrasia.

Ili kujenga jamii salama, familia zenye afya, kufikia mustakabali bora kwa vijana wa Tanzania, ni muhimu kuendelea kupanua nafasi ya ushiriki wa wananchi. Wananchi wa Tanzania ndio hazina na rasilimali kubwa zaidi ya nchi hii, na tunajivunia kushirikiana nao kuunga mkono mageuzi makubwa ya Tanzania.

Tunamaliza mwaka wa 2023 kwa furaha, kwani Shirika la Changamoto za Milenia (Millennium Challenge Corporation - MCC) limeichagua Tanzania kupata ruzuku kwa ajili ya maandalizi ya programu ya awali (threshold program) itakayoisaidia Tanzania kufikia malengo ya kiuchumi na ya kimageuzi, itakapokuwa ikijiandaa kwa uwekezaji mkubwa zaidi na uwezekano wa makubaliano kamili na MCC (MCC compact).

Ni nchi chache sana duniani zinaweka kipaumbele katika suala la amani na utulivu kama sehemu ya tunu zake kuu, kama wafanyavyo Watanzania.

Tunashukuru kwa ushirikiano wetu wa kijeshi unaodhihirika kupitia Mafunzo ya Pamoja ya Kubadilishana ujuzi na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na kuanza kwa ujenzi wa kambi mpya katika Chuo cha Intelijensia cha Jeshi la Ulinzi la Tanzania.

Wema na ukarimu wa Tanzania unatugusa sisi sote hapa ubalozini na unatupa hamasa ya kutekeleza programu za kimkakati na zenye ufanisi ambazo zitaimarisha urafiki wa muda mrefu baina ya mataifa yetu kwa siku nyingi zijazo.

Wakati msimu wa likizo na sikukuu unapoanza na tunapoutazamia mwaka mpya, sisi katika Ubalozi tunawatakia Watanzania wote amani na baraka tele, pamoja na afya njema na ustawi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga usajili makini unahitajika kufuzu robo CAF

**SHIRIKISHO** la Soka nchini (TFF), limeshatangaza kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili tangu Desemba 16, mwaka huu, huku likitarajiwa kufungwa Januari 16, mwakani.

Dirisha hilo ni maalumu kwa timu zote kuboresha vikosi vyao kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, ingawa kulingana na mwingiliano mkubwa wa ratiba baadhi ya timu bado hazijamaliza mzunguko wa kwanza, lakini hilo haliwezi kuzizuia kubaini idara zao zinazohitaji kuboreshwa katika dirisha hili.

Moja ya sababu zilizochangia kushindwa kukamilisha mzunguko wa kwanza ni kutokana na miamba ya soka nchini, Simba na Yanga kubanwa na ratiba ya michuano ya kimataifa Ligi ya Mabingwa Afrika na ile ya African Football League (AFL), ambayo Simba pekee kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki ilishiriki.

Hata hivyo, pamoja na timu kupata fursa kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara, lakini kufunguliwa kwa dirisha hilo ni nafasi muhimu kwa Simba na Yanga kujiimarisha kwa kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba na Yanga kwa sasa zinashika nafasi ya pili kila moja kwenye kundi lake la michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Katika Kundi B, Simba ipo nafasi ya pili ikiwa na pointi tano, nyuma ya kinara Asec Mimosas ya Ivory Coast yenye alama 10 huku Jwaneng Galaxy ya Botswana ikifuatia kwa alama nne na Wydad Casablanca ya Morocco ikiburuza mkia kwa pointi zake tatu.

Kwa upande wa Yanga kwenye Kundi D, nayo ina pointi tano sawa na kinara Al Ahly ya Misri, ambayo ina faida ya mchezo mmoja mkononi dhidi ya Belouizdad ya Algeria iliyopo nafasi ya tatu na pointi zake nne sawa Medeama ya Ghana inayoburuza mkia.

Hivyo, kwa nafasi walizopo wawakilishi hao wa Tanzania kwenye michuano hiyo ya CAF, tunaamini endapo watafanya usajili makini na wa malengo kwa kuzingatia ugumu wa mashindano hayo, wanaweza kutinga robo fainali na hata nusu kama si fainali kabisa.

Bado nafasi ipo wazi kwa kila timu kwenye makundi ya wawakilishi hao wa nchi, hivyo ni wakati mwafaka sasa kwa Simba na Yanga kulitumia vema dirisha hili kufanya usajili wa viwango kwa kumulika maeneo ambayo yahitaji kuongezewa nguvu ili kufanya vizuri katika michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Sisi Nipashe kama wadau wabobevu kwenye tasnia hii ya michezo, kwa namna tulivyowatazama wawakilishi hao wa nchi wakati wakicheza michezo yao katika michuano hiyo, tunaamini kwa Simba inahitaji kuongeza nguvu katika idara ya kiungo mkabaji na ikiwezekana mshambuliaji mmoja zaidi huku Yanga ipaswa kusaka mshambuliaji asili (namba tisa) kwa udi na uvumba.

Hayo ni maeneo muhimu kwa timu hizo kuanza kuyamulika kwa umakini kama zinataka kufanya vizuri katika mechi zao za raundi ya tano na sita na hatimaye kufuzu robo fainali.

Ni wazi mabenchi ya ufundi ya timu hizo tayari yameona mapengo hayo na kutoa mapendekezo bora kwa uongozi namna ya kuyaziba kwa kumulika wachezaji wenye viwango stahiki vya kuweza kushindana katika michuano hiyo.

Hivyo, hatutarajii kuona timu hizo zikifanya usajili wa wachezaji wengi usio na tija katika dirisha hili dogo, ambao utazifanya kuanza kujijenga upya, badala yake tunataka kuona maboresho ya kimalengo na kimkakati zaidi kuwea kufikia malengo yao msimu huu.

Pamoja na kwamba tunatambua katika dirisha hili dogo ni vigumu kupata wachezaji bora sokoni, ambao kanuni zitawaruhusu kucheza michuano hiyo, bado tunaamini zikitumia maskauti wazuri hili linawezekana kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Simba ikomeshe tatizo sugu la utovu nidhamu kwa wachezaji

**WIKI** hii Klabu ya Simba ilisimamisha wachezaji wake wawili, Clatous Chama na Nassor Kapama kwa utovu wa nidhamu.

Taarifa ya klabu hiyo ilieleza kutokana na vitendo vya utovu wa nidhamu, hivyo watapelekwa kwenye Kamati ya Nidhamu kwa hatua zaidi. Kamati hiyo ipo chini ya Mwenyekiti, Suleimani Kova, ambaye ni Kamanda mstaafu wa Jeshi la Polisi.

Hakuna yeyote ajuaye ni utovu upi wa nidhamu wa aina gani ambao wameufanya zaidi ya viongozi wa klabu hiyo, ingawa kwa vyanzo mbalimbali vinasema Chama alionekana kutotii mazoezi ya viungo yaliyokuwa yakitolewa na mmoja wa makocha wasaidizi Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, muda mfupi tu kabla ya mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca uliochezwa Jumanne iliyopita.

Lakini yapo mengine tena yanasemwa, ili mradi tu kila mmoja anaongea lake na hii yote ni kwa sababu klabu haikuainisha makosa ya wachezaji hao.

Kwa haya yote yaliyotokea na uchunguzi mdogo, nikipata taarifa za hapa na pale kutoka kwa baadhi ya watu wa karibu na klabu, inaonekana kuna tatizo la kutokuwapo kwa nidhamu kwa baadhi ya wachezaji wa klabu hiyo wanaoitwa au kujiita mastaa na si leo tu ila kwa muda mrefu.

Na hawa ndiyo wanaoeneza sumu kwa wenzao, hasa kwa wachezaji wapya na wale ambao hawana majina makubwa.

Binafsi, naona kuwa kuna baadhi ya wachezaji Simba ni kama 'miungu watu' kwani wana uwezo wa kufanya chochote na wasifanywe lolote.

Nafikiri hili lililofanywa sasa inawezekana ni matokeo tu ya ujio wa kocha mkubwa, mwenye msimamo mkali, Abdelhak Benchikha. Nadhani kama isingekuwa yeye, hata hili la wachezaji kusimamishwa kwa utovu wa nidhamu lisingekuwapo.

Inaonekana kama vile baadhi ya wachezaji wamekuwa na tabia hiyo muda mrefu, lakini wameachwa, wamezoea na hakuna mtu wa kumfunga paka kengele.

Uchezaji wa Simba kabla ya ujio wa Benchikha ulikuwa unatia wasiwasi kama wachezaji wa timu hiyo wanafanya mazoezi ya kutosha kweli chini ya kocha aliyeondoka, Robertinho Oliveira.

Kuna mtu aliniambia kuwa Robertino alikuwa amewekwa kiganjani mwa wachezaji mastaa ambao walikuwa wakimgomea kocha wa viungo aliyeondoka mazoezi anayotoa, kiasi kwamba inafikia wakati yanabadilishwa.

Ndiyo maana ilionekana timu haina stamina wala pumzi, lakini ujio wa kocha mpya kwa muda mfupi tu unaona angalau kikosi kina mabadiliko.

Halafu nikaambiwa kuwa wapo baadhi ya wachezaji hawataki kukaa kambini, badala yake wanakuja asubuhi na magari yao.

Nilishawahi kusikia pia kuwa kuna mchezaji alilirudisha basi la wachezaji nyuma ili liende kumchukua njiani baada ya yeye mwenyewe kuchelewa.

Dereza huyo aliamua kugeuza na kumfuata alipo wakati imeshaamriwa kuwa mchezaji akichelewa atafute usafiri wake wa kumpeleka mazoezini.

Baada ya mechi dhidi ya Yanga, Simba ikifungwa mabao 5-1, Kiongozi wa zamani wa Simba, Ismail Aden Rage, hakumung'unya maneno, akasema siku moja kabla ya mechi kuna baadhi ya wachezaji hawakulala kambini, walirejea asubuhi na akashangaa jioni wakapangwa kwenye mechi, alisema huo ni utovu wa nidhamu wa hali ya juu na kuwalaumu viongozi kwa kutokuchukua hatua za haraka.

Kwa mlolongo huu unaonesha kuna matatizo hayo, lakini pia kuna udhaifu kwa viongozi kuchukua hatua tangu mwanzo, hivyo mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

Nimpongeze kocha Banchikha kwa kuanza kurejesha nidhamu ndani ya timu na kambi, kwani bila hivyo hakutokuwa na mafanikio yoyote.

Pia niwashauri viongozi wa Simba waache tabia ya kukumbatia wachezaji wanaojiona mastaa kwani wanaongoza taasisi ambayo wachezaji, viongozi wanapita, wanaobaki ni wanachama na mashabiki tu.

Inawezekana labda viongozi walikuwa wanawaogopa mashabiki kwani baadhi ya wachezaji wanafanya hivyo huku ngao yao kubwa ikiwa ni kupendwa na mashabiki, na mastaa hao wamekuwa wakitumia kama kinga ya kujifichia kwenye uovu wao.

Simba wameshapita wachezaji wengi tangu enzi na enzi waliokuwa nyota na kuibeba timu hiyo, kama Abdallah Kibadeni, Zamoyoni Mogella, Malota Soma, Mohamed Mwameja, Juma Kaseja, marehemu Patrick Mafisango, Joseph Kaniki, Meddie Kagere, Emmanuel Okwi, lakini leo hawapo na timu inasonga mbele.

Hata wanaoitikisa wanapita na kuja wengine, hivyo viongozi waache kukumbatia wachezaji watovu wa nidhamu kwa sababu ya ustaa wao.

# Kihenzile ataka ‘speed’ ujenzi boti Ziwa Victoria

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile amelitaka Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), kuhakikisha mradi wa ujenzi wa boti yenye vifaa vya matibabu unakamilika kwa wakati na viwango.

Amesema kukamilika kwa wakati kwa mradi huo kutawawezesha wakazi wa Ziwa Victoria na visiwa vyake kuanza kutumia huduma hiyo.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki mkoani hapa wakati wa utiaji saini mkataba huo baina ya TASAC na kampuni ya LOCA Muhendislik Gemi Mak. PLas Ve Gd. San Tic ltd Sti ya nchini Uturuki.

Kihenzile alisema kukamilika kwa mradi huo kutarahisisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi na watumiaji wa usafiri majini hususani nyakati za majanga.

“Serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri kwa wananchi wanaotumia Ziwa Victoria na kupitia mradi huu sasa wa boti yenye vifaa tiba kutaokoa watumiaji wa usafiri wa majini na wananchi kwa kupata huduma za afya inapotokea ajali katika Ziwa Victoria,” alisema Kihenzile.

Pia, alisema pamoja na uwezeshaji wa mradi huo kwa sasa serikali iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Utafutaji na Ukoaji ambacho kitafanya kazi kwa ushirikiano na kituo cha Dar es Salaam ili kuimarisha usalama katika usafiri majini.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuimarisha usafiri huo kwa kuwekeza katika ujenzi wa meli na maboresho ya miundombinu, lengo likiwa kuchagiza uchukuzi katika Ziwa Victoria.

Makilagi alisema, mradi huo umekuja wakati mwafaka kwa kuwa kukamilika kwake kutachangia kuokoa maisha ya wananchi na kupata huduma hiyo kwa wakati.

Mwenyekiti wa Bodi ya TASAC, Nahodha Musa Mandia, alimhakikishia Naibu waziri kuwa bodi na menejimenti zimejipanga kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati na viwango.

Mradi wa ujenzi wa boti yenye vifaa vya matibabu unatarajiwa kugharimu Shilingi bilioni nne na unatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja.




Mratibu wa Taasisi ya Silver Crescent Tanzania, Kadir Komurcu (kulia), akifungua maji kwenye uzinduzi wa mradi wa kisima kirefu katika kijiji cha Mbaramo, wilayani Muheza juzi, kilichochimbwa kwa msaada kutoka Uturuki. Visima vitano vimechimbwa vijiji tofauti vyenye thamani ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kusaidia wananchi kupata majisafi na salama bure. Kushoto ni Mratibu wa taasisi hiyo, Tanga, Omari Shariff. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwekezaji amaliza mgogoro ulioibuliwa na TAWOMA

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

KUTOKANA na mgogoro ulioibuka wa Chama cha Wachimbaji Wanawake Mkoa wa Simiyu (TAWOMA), mwekezaji wa mgodi namba 10, Daudi Emmanuel, amesema hakushirikishwa, hata hivyo wamekaa na kumaliza tofauti hizo.

Ameridhia wachimbaji hao kuendelea na shughuli za uchimbaji baada ya kukubaliana kumaliza mgogoro unaodaiwa ulichangiwa na siasa.

Emmanuel akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu suala hilo mkoani humo, aliwasihi waache kutumiwa na wanasiasa wasioitakia mema nchi, kwasababu wao walitambua kwamba hawakuwa na leseni ya eneo hilo la mgodi.

Hatua ya wachimbaji kumwomba radhi mwekezaji huyo, wameruhusiwa kusimamia na kuendelea na uchimbaji katika mgodi huo na atakuwa akipokea taarifa za uendeshaji wa mgodi kutoka kwao na meneja wake.

“Naomba ifahamike kuwa hakuna mgogoro uliokuwapo kati yangu na wachimbaji hawa, mimi nawapenda sana wachimbaji wanawake wa Mkoa wa Simiyu.

Nimewapa ruhusa ya kusimamia mgodi, nitakuwa nikipokea taarifa za uendeshaji kutoka kwao,” alisema Emmanuel na kuongeza:

“Nawaomba sana wachimbaji wasikubali kutumiwa na wanasiasa wasiokitakia mema chama.

Kama kuna mambo ya msingi ni vema tukaketi pamoja tukazungumza ili kuondoa migogoro isiyokuwa na tija na pia endapo mtashindwa kuelewana ama mkipigana tena kwa sababu ya usimamizi sina budi kuwaondoa katika usimamizi ili mbaki kuwa wachimbaji tu.”

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Emmanuel Silanga, alisema kuwa kutatuliwa kwa mgogoro huo ni juhudi za kuunga mkono jitihada za serikali katika kuwawezesha kinamama ili kujiinua kiuchumi kwa maendeleo ya taifa.

“Serikali haipendi kuona kinamama wakiwa wanahangaika kwa sababu wao ndio uti wa mgongo wa familia ndio maana tunatamani kuona wakiwa vizuri kiuchumi kwa manufaa ya taifa la sasa na kesho kwa sababu wao ndio walezi wakuu wa familia, serikali inawajali ndio maana imeamua kusimamia hili ili kuhakikisha hakuna mgogoro tena,” alisema Silanga.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, akizungumzia suala hilo, alisema wameketi pamoja kati ya mwekezaji huyo na wachimbaji wanawake na amekubali kuwaruhusu kusimamia mgodi huo.

Baada ya kuruhusiwa kusimamia mgodi huo na kuendelea na kazi zao za uchimbaji wa dhahabu, Mwenyekiti wa TAWOMA, Mary Chacha, alimshukuru Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, Emmanuel Silanga, kwa kuwasaidia kurejea katika majukumu yao ya usimamizi wa mgodi na kwamba wamempongeza kwa kuwajali wachimbaji wanawake wa Mkoa wa Simiyu.

“Kwa niaba ya wanawake wachimbaji napenda kumshukuru Silanga kwa kutusaidia katika kumaliza huu mgogoro kwa njia nzuri ya maridhiano ya pande zote mbili na sisi turejea katika majukumu yetu tunamshukuru sana yeye pamoja na Mkuu wa mkoa kutusaidia katika hili,” alisema Chacha.

Hivi karibuni wachama wa TAWOMA Simiyu, waliadamana, kufanya fujo iliyowalazimu kuomba radhi kwa mwekezaji na kuendelea na shughuli za uchimbaji.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Ahukumiwa miaka 10 kwa kubaka, kuua

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Mtaa wa Kineng'ene, Manispaa ya Lindi, Simoni Omari (30) amehukumiwa kwenda jela miaka 10 na miezi mitano kwa kosa la kumuua Mwanahawa Mandula (50).

Hukumu hiyo imetolewa na Jaji Rose Ebrahimu wa Mahakama Kuu Kanda ya Mtwara, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa hukumu hiyo, Jaji Rose alimuuliza Mwanasheria wa Serikali, Nofard Setta kama ana kumbukumbu ya makosa ya nyuma yaliyowahi kutendwa na mtuhumiwa na kujibu hana, huku akiomba apewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine. Baada ya maelezo hayo, wakili Issa Chiputula aliyekuwa anamtetea mshtakiwa huyo, aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu mteja wake akisema bado ni kijana, pia kitendo cha kukaa mahabusu muda mrefu imemwathiri kisaikolojia na hakuisumbua mahakama, hivyo anajutia kutenda kosa hilo.

Awali ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali kwamba Aprili 13, 2021 katika eneo la Kinengene Halmashauri ya Lindi, mshtakiwa alimuua Mwanahawa Mandala kwa kumpiga na silaha yenye ncha kali maeneo mbalimbali ya mwili wake.

Ilidaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alitekeleza tukio hilo baada ya kuombwa na Mwanahawa kwenda shambani kumlimia na walipofika mshtakiwa akaomba apewe penzi.

Taarifa zaidi zinadai kuwa mshtakiwa alipokataliwa ndipo akatumia nguvu na kubaka kisha kutekeleza mauaji hayo.

Mwanasheria huyo alidai kwamba mwili wa marehemu uliokotwa na wananchi waliokuwa wakipita njia ukiwa unatoka damu puani na masikioni na majeraha maeneo mbalimbali ya mwili.



Kazi ya upanuzi wa barabara kuanzia eneo la Mlimani City kuelekea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiendelea. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima wafundwa nidhamu matumizi ya fedha

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

WAKULIMA mkoani Lindi wametakiwa kuzingatia mambo muhimu wanapopata fedha baada ya kuuza mazao yao ikiwamo kuwapeleka watoto shule.

Rai hiyo imetolewa juzi na Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika (RUNALI), Odas Mpunga, wakati akizungumza na wakulima kwenye mauzo ya mnada wa mwisho wa korosho msimu wa mwaka huu uliofanyika mjini Nachingwea, wilayani hapa.

Akizungumza baada ya mnada huo na wakulima kuridhia kuuza korosho walizopeleka ghalani kwa bei ya juu Sh. 1,650 na ya chini Sh. 1,550, aliwakumbusha kutumia fedha wanazozipata kununua chakula na kuwasomesha watoto.

Mpunga aliwakumbusha kujenga nyumba bora za kuishi na waachane na tabia ya kuendelea kuishi katika nyumba za tembe zilizojengwa kwa udongo na kuezekwa kwa nyasi.

"Fedha tunazopata zitubadilishe kuishi kwenye nyumba nzuri na siyo zile za udongo zilizoezekwa kwa nyasi. Hizo nyumba zinakaribisha wadudu ikiwamo nyoka," alisema Mpunga.

Pia aliwataka kusomeshea watoto kwa kuwanunulia vifaa vya shule na kujielekeza katika kulima mazao ya chakula na kujiwekea akiba ya chakula ili kuondokana na tatizo la baa la njaa.

# Wavuvi watishia kugoma kulipa ushuru kisa ubovu paa la soko

**Na Said Hamdani,** LINDI

UMOJA wa wavuvi na wachuuzi wa samaki wabichi katika Manispaa ya Lindi, wametishia kufanya mgomo wa kutolipa ushuru unaotozwa na halmashauri hiyo hadi pale uongozi utapokarabati paa la jengo.

Wamesema paa hilo ni chakavu hali inayosababisha kuezuliwa na upepo mara kwa mara.

Mwenyekiti wa umoja huo, Salehe Kazumali, alisema hayo katika barua waliyoandika kwenda Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Lindi, Juma Mnwele, wakieleza adhma ya kufanya mgomo baada ya kupata adha kila wakati wanapotekeleza majukumu yao sokoni.

Barua hiyo ambayo Nipashe iliona nakala yake, iliandikwa Desemba 18, mwaka huu na kusainiwa na mwenyekiti wao, Salehe Kazumali.

Sehemu ya barua hiyo inamtaka mkurugenzi huyo kutekeleza ahadi aliyoahidi ya kurejesha paa hilo ifikapo Desemba 10, mwaka huu.

Aidha, inaeleza kwamba kutokana na tatizo hilo wavuvi na wachuuzi wa samaki wabichi wanapata mateso makubwa ya kunyeshewa mvua na kupigwa na jua wanapokuwa kwenye majukumu ya kila siku ya kuuza na kununua samaki katika soko hilo.

"Tulifika ofisini kwako kuwasilisha kilio chetu na kutuahidi hadi Desemba 10 kazi hiyo itatekelezwa, lakini muda unazidi kupita hakuna kinachoendelea," ilieleza sehemu ya barua hiyo.

Aidha, barua hiyo inaeleza kuwa ifikapo Desemba 25, mwaka huu, bila kuona utekelezaji wake watatoa tamko la kuwataka wavuvi na wachuuzi kutolipa ushuru wanaotozwa wa asilimia tatu hadi pale watapojengewa sehemu ya hifadhi.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, akijibu malalamiko ya wavuvi hao, kupitia barua kumbukumbu Na. LMC/M 10/86/128 ya Desemba 19/2023 na kusainiwa na Juma Mnwele, ameuomba uongozi kutozuia ulipaji ushuru kwa kuwa kazi ya urejeshaji paa itafanyika ndani ya muda uliopangwa.

Alisema pamoja na matatizo yaliyopo halmashauri ina jukumu la kutengeneza mazingira wezeshi ya kufanya biashara kwa makundi mbalimbali yakiwamo yanayotumiwa na wachuuzi wa samaki wabichi.

"Ninapenda kukufahamisha ukarabati wa eneo lililoezuliwa na upepo utafanyika ndani ya muda kama ilivyoahidiwa," ilieleza sehemu ya barua hiyo.





Watoto wa Zaina Kipanga, Mariamu na Mkiwa wakikusanya mabaki ya mahindi yanayodaiwa kufyekwa na viongozi wa serikali ya kijiji cha Kwamsisi wilayani Korogwe, mkoani Tanga mwishoni mwa wiki.
**PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Wagonjwa 300 kupatiwa tiba ya mtoto wa jicho Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

TAASISI ya Silver Crescent ya Uturuki, imepiga kambi maalum katika Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, kwa ajili ya kufanya uchunguzi na tiba ya upasuaji wa macho kwa wagonjwa 300 wa mtoto wa jicho (cataract), waliojitokeza kutoka maeneo mbalimbali.

Akizungumzia kambi hiyo, Mratibu wa Silver Crescent, Mkoa wa Tanga, Omari Shariff, alisema kambi hiyo ya siku, itahusisha pia utoaji wa miwani za jua kwa waliochunguzwa na kukutwa na matatizo katika uoni.

Kwa mujibu wa Shariff, kambi hiyo ya uchunguzi wa macho, upasuaji wa mtoto wa jicho na kutoa miwani kwa wagonjwa, imeigharimu taasisi hiyo zaidi ya Sh. milioni 36.

Kambi hiyo iliyowekwa katika Kituo cha Afya cha Ubwari, ilizinduliwa juzi na Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma.

Katika hotuba yake, Naibu Waziri huyo, alisema dhamira ya serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kushirikiana na wadau wa huduma za macho ndani na nje ya nchini kufuata vipaumbele vya Wizara ya Afya kwa kuwafikia wananchi kwa ukaribu zaidi kwa kutumia huduma mkoba.

Katika hatua nyingine, Silver Crescent ya Uturuki, imekabidhi pia mradi wa maji wa visima virefu vitano ilivyochimba katika vijiji vya Sega, Lusanga, Genge, Mbaramo na Majengo ili kuwasaidia wakazi wake kuepukana na adha ya ukosefu wa majisafi na salama.

Mratibu wa Taasisi hiyo nchini, Kadir Komurcu, alisema msaada huo uliogharimu Sh. milioni 500 ni utaratibu wa kawaida wa taasisi hiyo, kusaidia jamii ili kuhakikisha wanapata majisafi na salama.

"Tumekuwa na utaratibu wa kusaidia jamii, kwa sababu ina watoto, wazee na jamii ya watu wenye ulemavu. Tuliguswa na kuona kwamba tukiwasaidia kupata maji, wataondokana na adha ya kuhemea maji usiku na mchana katika vijiji jirani," alisema Komurcu.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Sega, Halima Juma, alisema wanajisikia faraja kupata maji waliyokuwa wakiyafuata na kupoteza muda mwingi badala ya kufanya shughuli za kiuchumi.

# RC atangaza vita kwa ma-DC ucheleweshwaji miradi ya elimu

**Na Allan Isack,** LONGIDO

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, amewanyooshea vidole wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri walipo kwenye maeneo aliyobaini kuna ucheleweshaji wa miradi ya elimu.

Aliwaagiza kuhakikisha miradi hiyo inakuwa tayari mpaka kufikia Januari 5, mwaka ujao na hatomvumilia kiongozi ambaye hatotekeleza agizo hilo ilhali pesa za ujenzi zilitolewa.

Mongela alitangaza vita hiyo mwishoni mwa wiki, baada ya kukagua ujenzi wa shule mpya maalum ya Sekondari ya Wasichana ya Orbomba iliyoko katika Wilaya ya Longido.

"Kwa shule ambazo nitabaini kulegalega kukamilika, wakati fedha za ujenzi zimetolewa kwa wakati, nitadili na wakurugenzi na wakuu wa wilaya, hakuna kingine,"alisema Mongela.

Hata hivyo, alisema serikali chini ya uongozi wa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, imetoa fedha Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo.

"Katika ujenzi wa shule hii mpya ya wasichana serikali imetoa Sh. bilioni tatu na kazi inaendelea vizuri lakini nimesisitiza kwa Mkuu wa Wilaya na timu yake kuongeza kasi ya ujenzi ikiwamo kuwaongeza mafundi ili kazi ikamilike kwa wakati," alisema Mongela.

Alisema ajenda ya serikali, ni kuhakikisha watoto wakike hasa wanaotoka kwenye jamii za kifugaji wanapata elimu bora na ya uhakika.

"Kama mnavyofahamu jamii yetu huku, kwa zaidi ya asilimia 99 ni ya kifugaji, na kwa asili ya jamii ya kifugaji, ni lazima tukiri kwamba watoto wa kike walibaki nyuma.

"Nasisitiza viongozi wa Wilaya ya Longido, kwa kuwa shule zinafunguliwa Januari 8 mwakani, ni lazima miundombinu ya elimu iwe imekamilika tayari, kwa ajili ya kupokea wanafunzi kama serikali ilivyolenga ili kupata thamani halisi ya uwekezaji huu."

Awali Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Orbomba, Surpeti Mseya, alitaja sababu zinazochangia kuchelewa kukamilika kwa mradi hiyo kuwa ni pamoja na mvua nyingi zilizonyesha eneo hilo.

"Mradi umechelewa kukamilika kutokana na kunyesha kwa mvua nyingi lakini kutokana na hali halisi ya udongo wa hapa kuwa laini magari yalishindwa kufika hapa, pia upatikanaji wa mawe ulikuwa adimu na uhaba wa maji,"

# Mkuu wa wilaya ahamasisha wananchi utalii wa ndani

**Na Hamida Kamchalla,** LUSHOTO.

MKUU wa Wilaya ya Lushoto Kalisti Lazaro, ametoa wito kwa wananchi wa ndani na nje ya wilaya hiyo kutembelea na kujionea vivutio vya utalii vinavyopatikana katika Hifadhi ya Msitu wa Asili Magamba.

Lazaro alitoa wito huo katika hifadhi hiyo na kusema wameandaa mashindano ya watembea kwa miguu pamoja na waendesha baiskeli kwa lengo la kuhamasisha utalii wa ndani kwa watalii kutoka nchi mbalimbali ili kukuza na kuunga mkono juhudi za serikali katika kuchangia pato la Taifa.

"Tumeanzisha shuhuli yetu hii ambayo tumeipa jina la Walkerthon and Adventure, ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Asili Magamba ambapo watu wametembea ndani ya msitu, watu wengi wa Lushoto hawajui kama wana rasilimali kubwa ndani ya Wilaya yao".

"Ni msitu wa zaidi ya mita za mraba 9000 na kuna vituo vingi vya utalii, kuna mabwawa, vinyonga, maporomoko ya maji lakini pia kuna ndege aina mbalimbali hivyo niwaombe watu wajitokeze kwa wingi kutembelea msitu wetu," alisema.

Kwa upande wake Mhifadhi Mwandamizi wa Hifadhi ya Msitu wa Asili Magamba (CSO), Christoganus Vyokuta, alisema uhamasishaji huo ambao umewashirikisha Ofisi ya mkuu wa wilaya pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umelenga kumuunga mkono Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kmpeni yake ya The Royal Tour.

"Kuanzia Disemba 16 mpaka kufikia tumeanza kuonesha vivutio vilivyoko ndani na wafanyabiashara ili kuhakikisha wananchi wanaifahamu vema wilaya yao lakini pia ikiwa ni juhudi za kuunga mkono utalii aliouanzisha Rais wetu," alisema.

Aidha alisema kuwa wako bega kwa bega na Ofisi ya mkuu wa Wilaya kuhakikisha kwamba kila kinachoanzishwa ngazi ya juu kinatekelezwa na kwamba kutakuwepo na mashindano mbalimbali katika matembezi hayo na mwamko wa washiriki ni mzuri.

"Katika mashindano haya wapo washiriki zaidi ya 130 ambao wamefanya matembezi kuanzia km 5, 10 na 15 na wapo pia washiriki wa baiskeli, lakini mbali na hili wapo watalii wa ndani na nje ya wilaya ambao wamelala ndani ya Hifadhi.

Vyokuta alibainisha kwamba zaidi ya Sh. milioni 200 zimetumika kuboresha na kunufaisha utalii katika Hifadhi ya Msitu wa Asili Magamba, fedha ambazo zilitokana na mradi wa Uviko 19.

"Maeneo yaliyofadhiliwa na mradi huu ni uboreshaji wa miundombinu ya utalii ikolojia katika Hifadhi ambayo imerahisisha watalii wa ndani na nje kufika kwa urahisi" alibainisha Vyokuta.

Hata hivyo alisema kuna matatizo kadhaa ambayo yanafanywa na binadamu katika uchafunzi wa mazingira kwenye eneo la uhifadhi ambayo yako kinyume na sheria huku akitoa wito kwa wananchi kuacha tabia zote ambazo kwa namna moja au nyingine yanaleta athari kwa Hifadhi hiyo. Alisema katika msimu wa kiangazi jamii zinazopakana na Hifadhi huwasha mioto kwa ajili ya shuhuli za kibinadamu, lakini pia kuna wananchi wachache wasio waaminifu kuingia hifadhini na kufanya shuhuli za uchimbaji wa madini na ukataji wa miti kinyume na sheria.

"Wizara ya Maliasili na Utalii tumerithishwa, tuwarithishe na tunashukuru serikali ya awamu ya sita kwa kushirikiana na wananchi kuhakikisha misitu yetu inatunzwa kwa faida ya kizazi cha sasa na baadaye" alibainisha.

# Ugumu wa maisha unavyoathiri sherehe Krismas na Mwaka Mpya Kanda ya Ziwa

**Na Waandishi Wetu**



Shughuli za kibiashara zikiendelea katika eneo maarufu la biashara za nguo na vitu mbalimbali la Makoroboi, lakini msimu huu watu ni wachache tofauti na inavyokuwa katika misimu mingine ya sikukuu. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

UGUMU wa maisha unaotajwa kusababishwa na kupanda kwa bidhaa na mabadiliko ya tabianchi unaelezwa kubadilisha utamaduni wa kusherehekea sikukuu za Krismas na mwaka mpya katika maeneo mbalimbali ya kanda ya ziwa.

Baadhi ya wananchi kutoka katika mikoa hiyo waliiambia Nipashe kuwa kupanda kwa bidhaa na ukosefu wa fedha vimesababisha kuziona siku hizo za kawaida na kupanga kwenda katika maeneo ya ibada kisha kurejea na kuendelea na shughuli za kila siku.

Mkazi wa Ihayabuyaga,Kisesa mkoani Mwanza Rhoda Alen, alisema analazimika kutosherehekea kama zamani ili kukidhi mahitaji mengine ya kifamilia ikiwamo kulipia ada za watoto.

Alisema mfumo wa maisha umebadilika hivyo hata ule utamaduni wa kualikana kula sikukuu pamoja limekuwa gumu kwa kuwa hakuna uwezo wa kugharamia chakula cha kuwalisha ulioaalika.

"Kwa sasa mtu badala ya kuchinja kuku mwenye thamani ya Sh.15,000 hadi Sh.20,000 au Mbuzi wa Sh.150,000 anaona ni bora fedha hiyo aitunze kwaajili ya maandalizi ya watoto shule na ni kutokana na vitu kuwa juu kulinganisha na kipato cha mtu,"alisema Emmanuel Kudema Mkazi wa Maswa.

Helenestina Juma Mkazi wa Rwamishenye mkoani Kagera alisema baadhi ya wananchi wanashindwa kumudu milo miwili kwa siku hivyo kutofikiria tena suala la sikukuu kwa kununua nguo, mbuzi, kuku wala kualikana.

Naye Claveri Kristopher kutoka mkoa huo alisema zamani walikuwa tukichanga fedha katika vikundi na kununua Ng'ombe katika sikukuu na kugawana ili kupata mboga katika siku hizo lakini kwa sasa mambo hayo yameisha kutokana na watu kukosa fedha.

Mkazi wa Manispaa ya Shinyanga, Manyanda Kitunda, alisema walizoea shamrashamra sikukuu zikikaribia lakini kwa sasa mpaka inafika hawana habari kutokana na uwezo wa kifedha.

"Hata utaratibu wa kuwanunulia nguo watoto na wazazi kushona nguo umeisha kabisa maana unaangalia kutoa Sh.17,000 kwaajili ya suruali ya mtoto na Shati Sh.10,000 na ukiangalia hakuna chakula unaona hiyo ngoja ipite tu,"alisema Ester Masunga Mkazi wa Shinyanga.

Huko wilayani Kahama wananchi wanataja kupanda kwa gharama za Maisha kumeharibu utamaduni wa watu kufanya maandalizi ya kununua mahitaji mbalimbali kwa kujumisha majirani ili kusherehekea pamoja wakitaja hali hiyo kuongeza uchoyo na ubinafsi katika siku hizo.

Akieleza utaratibu wa sikukuu za nyuma bi. Esther Mwijarubi (62) alisema walizoea kufunga safari kutembelea ndugu kusherehekea pamoja hali iliyosaidia ndugu kufahamiana tofauti na sasa kila mtu anafanya vitu nyumbani kwake.

Mkurugenzi wa kituo cha kulelea watoto wenye mahtaji cha Juniors and Child Foundation kilichopo wilayani Maswa, Joseph Jidayi, aliiambia Nipashe kuwa kipindi hiki hakuna mwitikio wa watu kushiriki na watoto hao kama ilivyo kwa miaka yote hali inayowakosesha faraja.

**BEI ZA BIDHAA SOKONI ZAPAA**

Bei za bidhaa mbalimbambali katika mikoa ya Kanda ya Ziwa imepanda ikiwamo Sukari kutoka Sh.2800 hadi 3500 kwa kilo moja, Lita ya Mafuta ikipanda kutoka Sh.5000 hadi Sh.7000 (Sh.24000-28000 kwa lita tano), nyama ikiuzwa Sh.8000 kutoka 7500.

Sado la nyanya limepanda hadi Sh.6000 huku nyanya moja ikiuzwa Sh. 200,kilo ya vitunguu Sh.3000, mbuzi Sh.150,000 hadi Sh.180,000 kutoka Sh.70,000 hadi Sh.90,000. Kreti la Soda linauzwa Sh.12,000 bei ya jumla kutoka 11800 na soda moja kuuzwa kwa Sh.700.

Aidha Mchele umeshuka kutoka Sh.3200 hadi 2600 mpaka 2200 zikitofautiana kulingana na eneo na ubora, Maharagwe yananunuliwa sawa na mwaka jana kwa Sh.2800, Viazi Mviringo vikishuka kutoka Sh.1200 hadi 1000.

**KILIO CHA WAFANYABIASHARA, WATOA HUDUMA**

Mwenyekiti wa Soko kuu Mjini Maswa mkoani Simiyu, Naftali Joram, alisema biashara imedorora kutokana na kukosa mwitikio wa wananchi licha ya bei za baadhi ya bidhaa kama nguo kuendelea kubaki vilevile.

Fundi cherehani kutoka Mjini Maswa Elizabeth Boniphace humo aliiambia Nipashe kuwa wateja wa kushona nguo za sikukuu hakuna kulinganisha na mwaka jana hivyo wanaishia kushona sale za Shule tu.

Fundi cherehani mwingine Mkazi wa kata ya Maliunga Manispaa ya Kahama, Mussa Husein alisema,mwezi mmoja kabla ya sikukuu alikuwa akipata tenda za kushona nguo mitindo mbalimbali kwa akinamama na watoto lakini kwasasa imekuwa tofauti na wamebaki kushona viraka kwenye nguo tu.

Kwa mujibu wa Alex Jumanne mmoja wa wafanyabiashara katika mnada wa Kisesa wilayani Magu anasema hali ya biashara kwa kipindi hiki si nzuri kulinganisha na mwaka uliopita kwani mnadani hakuna wateja kama ilivyozoeleka.

Paulo Kazimili Mfanyabiashara wa nyama mkoani Mwanza alisema bila kuwa na Sh.300,000 hauwezi kupata ng'ombe huku huku nyama ikipanda bei kutoka Sh. 8000 hadi 9000.

Mfanyabiashara wa kuuza nguo soko la Bukoba Audax Elpidius alisema,"licha ya kuleta nguo mpya nilitegemea kuwa nitauzia watu kwani msimu huu huwa tunategemea kufanya sana biaashara lakini tangu nimeleta mzigo nimeuza nguo tatu pekee za watoto."

"Kwa kweli msimu wa mwaka huu unaonekana kuwa mgumu zaidi ya ukilinganisha na miaka iliyopita huwezi kuamini tangu nimefungua duka langu saa 2 asubuhi hadi saa sita hii sijauza nguo hata moja,"amesema Levina Rwezahula Mfanyabiashara kutoka Chato mjini.

Makache Charles Muuza nyama alisema upo uwezekano mkubwa wa kutochinja nyama ya ng'ombe siku ya sikukuu ya krisimas kutokana na ugumu wa biashara uliopo kwa sasa,ambapo ng'ombe mmoja anachinjwa na kugawanywa kwenye maduka matatu tofauti.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa baadhi ya wafanyabishara,wauzaji wa mboga mboga wameonekana kufurahia biashara yao kwa madai ya wateja kuongezeka kila uchao na kuuza mafungu zaidi ya 30 hadi 50 kwa siku.

**WATAALAM WA UCHUMI WANENA**

Mchumi na Mhadhiri kutoka chuo kikuu SAUT kampasi ya Mwanza, Dk. Isack Safari alisema mfumko wa bei ulikuwepo hata katika sikukuu za miaka ya nyuma lakini kukosekana kwa fedha katika mifuko ya watu ndiyo sababu kwa mwaka huu kuonekana hali ni ngumu zaidi.

Jonathani N'handi Mnyela Mtaalamu wa Uchumi Tumizi(Applied Economist) wilayani Maswa alisema hali hiyo inatokana na uhalisia wa kipato na matumizi cha kila Mtanzania hivyo hali hii inasababiswa na kipato kidogo kulinganisha na hali ya maisha ilivyo kwa sasa.

Mtaalamu mwingine wa uchumi kutoka wilayani Sengerema Damian Mosha alitaja uhaba wa bidhaa sokoni na uhitaji unakuwa mwingi hivyo lazima vitu vipande bei maana matumizi yanaongezeka na kusababisha ongezeko la bei.

**MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**

Mtakwimu Mkuu wa Serikali Dk. Albina Chuwa aliambia Nipashe kuwa mfumuko wa bei unaendelea kuwa na tarakimu moja ambayo ni 3.2 huku chakula kikishika nafasi ya juu kwa kuwa na asilimia 28.2 licha ya kuwa bado kipo cha kutosha.

"Sasa hivi tunavuna mboga za majani tunakula kwa wingi mahindi mabichi yamejaa hivyo bado mfumuko wetu wa bei unaendelea kudhibitiwa vizuri,"alisema Dk.Chuwa

**Imeandaliwa na Shaban Njia (KAHAMA), Alex Sayi (MASWA), Restuta Damian (KAGERA), Daniel Limbe (CHATO), Elizabeth Seleman (SENGEREMA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Neema Emmanuel (MWANZA), Vitus Audax (MWANZA)**

Nipashe
Spotika



MAKIPA 10 BORA WA WAKATI WOTE 14



HARRY KANE

# NYOTA WA5 BORA DUNIANI KWA SASA

**LONDON,** England

KWA sasa tupo msimu wa likizo wa 2023-24, tumejipanga kwa ajili ya michezo mikali ya soka katika miezi michache ijayo. Ligi Kuu za Ulaya pamoja na Ligi ya Mabingwa sasa ziko katika mkondo kamili na mashabiki wengi sasa wanaangalia namna klabu zao zinavyoweza kujipaisha kwenye kipindi kilichobaki cha msimu.

Ni wakati wa programu sasa kujumuisha kiwango cha msimu wa mapema tunapoelekea sehemu ya kati ya kampeni. Kama msemo unavyokwenda, wakati mambo yanapokuwa magumu, wagumu wanaenda.

Bila kuchelewa zaidi, hebu tuangalie wachezaji watano walio katika kiwango bora sana duniani kwa sasa...

**#5 Cristiano Ronaldo (Al-Nassr)**

Itakuwa kosa la jinai kuangalia namba za Cristiano Ronaldo msimu huu na kumwacha nje ya orodha hii. Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or sasa ana umri wa miaka 38 na hana kazi ya kuwa bora kama alivyo katika hatua hii ya mwisho ya kazi yake.

Ronaldo ndiye kinara wa mabao kwenye Ligi Kuu Saudi Arabia akiwa amefunga mabao 15 katika mechi 14 alizocheza. Amefunga mabao nane na kutoa asisti moja katika mechi zake 10 zilizopita kwenye mashindano yote kwa klabu na nchi. Ronaldo bila shaka ni mmoja wa wachezaji walio katika kiwango bora zaidi duniani kwa sasa.

**#4 Trent Alexander-Arnold (Liverpool)**

Trent Alexander-Arnold bila shaka ni mmoja wa walinzi bora wa kizazi chake. Safu ya ulinzi kwenye mchezo wa Mwingereza huyo inakosekana wakati fulani, lakini anaifanya zaidi ya uwezo wake ubunifu na ufundi kwenye mpira.

Alexander-Arnold amekua katika kiwango bora wiki za hivi karibuni na amekuwa mleta tofauti kwa Liverpool hivi karibuni. Amekuwa imara msimu mzima, lakini anaonekana kuwa anapiga hatua yake ipasavyo sasa.

Trent amefunga mabao mawili na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi zake nne zilizopita kwa 'Wekundu' hao.

**#3 Kylian Mbappe (Paris Saint-Germain)**

Baada ya msimu wa thamani wa 2022-23 katika kiwango cha mtu binafsi, Kylian Mbappe ameanza tena huduma za kawaida kwa Paris Saint-Germain kwa mara nyingine tena muhula huu. Bila shaka ni mshambuliaji mahiri zaidi wa kizazi chake, Mbappe amepiga gia ya juu katika wiki za hivi karibuni.

Mbappe amefunga mabao tisa na kutoa pasi za mabao kwenye mechi sita zilizopita katika michuano yote kwa klabu na nchi. Usafirishaji huu wa kuvutia katika wiki tatu zilizopita unajumuisha hat-trick mbili. Mbappe anaonekana kuwa na msimu mwingine bora.

**#2 Jude Bellingham (Real Madrid)**

Jude Bellingham amekuwa mmoja wa wachezaji wanaovutia zaidi katika ligi tano bora za Ulaya katika msimu wa 2023-24. Kinachofanya uchezaji wake katika hatua za mwanzo za kampeni mpya kuvutia zaidi ni kwamba amefanya katika klabu yake mpya ya Real Madrid.

Bellingham alijiunga na Real Madrid kama mchezaji wao wa pili ghali zaidi kwa wote msimu huu wa majira ya joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akiwachezea 'Los Blancs' hao msimu huu na amekuwa mchezaji wao bora hadi sasa.

Katika mechi zake 10 zilizopita kwenye mashindano yote kwa klabu na nchi, Bellingham amefunga mabao nane na kutoa asisti tatu.

**#1 Harry Kane (Bayern Munich)**

Akiwa ameachana na minyororo iliyomzuia Tottenham Hotspur, Harry Kane anaonekana kudhamiria kushinda baadhi ya zawadi bora msimu huu. Bila shaka ni mchezaji aliye katika kiwango bora zaidi kwenye ligi tano bora za Ulaya msimu huu.

Kane ameonesha uwezo wake wa kufunga mabao katika hatua za kampeni mpya. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amekuwa akifunga mabao kwa katika kila mechi na yakufurahisha.


Ametikisa nyavu mara 14 na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi 10 zilizopita kwenye mashindano yote kwa klabu na nchi. Iwapo Kane ataweza kuboresha hili, Bayern Munich itaweza kutoa changamoto kubwa sana msimu huu.

Shukrani kwa kiwango chake cha ajabu cha kufunga mabao, inaweza kusemwa kwamba 'Bavaria' hao kwa sasa wameweza kumpata Robert Lewandowski mpya.

## ISIKUPITE

WACHEZAJI watano wenye tuzo nyingi za Mchezaji Bora wa Mechi katika soka ni

**#1 Lionel Messi (395),**
**#2 Cristiano Ronaldo (176),**
**#3 Zlatan Ibrahimovic (116),**
**#4 Eden Hazard (100) na**
**#5 Robert Lewandowski (96).**



# WACHEZAJI WA5 WALIOREJEA KWENYE UBORA MSIMU HUU



RONALDO

**LONDON,** England

KIWANGO ni jambo muhimu sana kwa wachezaji katika kiwango cha juu cha mchezo. Mechi huamuliwa na aina ya wachezaji, kwa pamoja au binafsi.

Kumtazama mchezaji akirejea katika kiwango chake cha juu ni tamasha linalojumuisha kiini cha ukombozi katika ulimwengu wa michezo. Furaha hiyo haitoki tu kutokana na uwezo wa ajabu wa mtu huyo bali pia kutokana na ushupavu na uthabiti walioonesha katika nyakati ngumu.

Inaletwa na muunganiko wa hali mbalimbali. Timu ya usaidizi, mazingira ya kukuza mafunzo na ukuaji wa binafsi na vyote vinaweza kutengeneza njia ya ufufuo kama huo. Kurudi kwenye kiwango ni ushuhuda wa roho ya mwanamichezo isiyoweza kushindwa.

Katika makala haya tunawaangalia wachezaji watano ambao wamerejea kwenye ubora wao msimu huu.

**#5 Isco (Betis Betis)**

Kati ya wachezaji wote ambao wamefurahia ukombozi msimu huu, Isco labda ndiye alitarajiwa zaidi. Alionekana kama mshindi wa dunia wakati wa miaka yake kuu pale Real Madrid. Mchezaji nyota wa safu ya kati wa Hispania alicheza na kuwapita wapinzani na kuonekana amerudi tena kwenye kiwango chake kama ilivyokuwa kule Madrid.

Hata hivyo, mambo yalimwendea mrama Isco mwaka 2018. Real Madrid ikaamua kumuuza kwa Sevilla katika msimu wa 2022-23. Hakufanya vizuri hapo hadi wakati anamaliza mkataba wake kwa makubaliano ya pande zote mbili mwishoni mwa Desemba.

Isco hakucheza kipindi cha pili cha muhula uliopita. Kwa hiyo, wakati Real Betis ilipompa mkataba wa mwaka mmoja msimu wa majira ya joto, ulimwengu wa soka haukumjali. Lakini Isco ameshangaza kunyakua fursa ya kukombolewa kwa ukali wa kiwango chake.

Ndiye tishio kubwa la ubunifu kwa Betis siku hizi na anaongoza kurejea kwenye soka la Ulaya msimu huu. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao matatu na kutoa asisti tatu katika mechi 21 kwenye michuano yote hadi sasa.

**#4 Virgil van Dijk (Liverpool)**

Uchezaji duni wa Liverpool msimu wa 2022-23, ulisababishwa na mambo kadhaa. Safu ya majeruhi, safu ya kiungo na baadhi ya wachezaji waandamizi kutocheza vizuri ndio sababu kuu za kufanya kwao vibaya msimu uliopita.

Virgil van Dijk alikuwa mkuu kati ya wachezaji walioshindwa kucheza kwa uwezo wao wote. Baada ya kuvuka hadi miaka yake ya 30, makubaliano yalionekana kuwa Mholanzi huyo sasa alikuwa akipungua. Lakini nahodha huyo wa Liverpool amezima dhana hiyo mapema katika kampeni mpya.

Amekuwa mtu muhimu katika kufufuka kwa Liverpool msimu huu. Van Dijk amekuwa akicheza nafasi kubwa nyuma ya 'Wekundu' hao na mchango wake umekuwa mkubwa katika kuwasaidia kwenye mbio za Ligi Kuu England

kuliko Trent Alexander-Arnold. Yeye si mahiri sana linapokuja suala la majukumu yake ya ulinzi, lakini kama chombo cha ubunifu, Mwingereza huyo ni tabaka tofauti.

Alipata mengi msimu uliopita huku Liverpool ikipambana. Lakini ni lazima ieleweke kwamba akiwa na kiungo mkongwe, Alexander-Arnold aliwekwa wazi sana wakati wa mabadiliko ya ulinzi. Kwa hiyo, mchango wake wa ulinzi, au ukosefu wake, umeonekana kuwa na upungufu mkubwa katika mchezo wake.

Lakini akiwa na safu ya kiungo iliyotiwa nguvu na sura mpya, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ameendelea kuonesha jinsi alivyo mchezaji mzuri. Amerejea kwenye ubora wake na amekuwa na nguvu ya kuhusishwa na upande wa kulia wa Liverpool.

Katika mechi 19 kwenye michuano yote, Alexander-Arnold amefunga mabao mawili na kutoa asisti tano.

**#2 Son Heung-min (Tottenham Hotspur)**

Akiwa na bao lake katika ushindi wa 4-1 wa Tottenham Hotspur dhidi ya Newcastle United mnamo Desemba 10, Son Heung-min alisawazisha mabao yake ya Ligi Kuu ya England kwa msimu wa 2022-23.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini alishiriki Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu na Mohamed Salah msimu wa 2021-22 baada ya kufunga mabao 23. Spurs kwa pamoja walikuwa duni muhula uliopita na kiwango cha Son pia kiliathirika.

Lakini amerejea katika ubora wake kwa mara nyingine tena na amekuwa mshambuliaji mkuu kwa upande wa kocha Ange Postecoglou msimu huu wa 2023-24.

**#1 Cristiano Ronaldo (Al-Nassr)**

Huwezi kumwacha mtu huyu, sivyo? Ulipofikiria wakati wa Cristiano Ronaldo, mmoja wa magwiji wa wakati wote wa mpira wa miguu kutundika buti ulikuwa umefika, ilikuwa ni kosa kufikiria hivyo. Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or amekuwa akitajwa msimu huu.

Ana umri wa miaka 38 sasa, lakini amekuwa akifunga mabao ya kujifurahisha kwa Al-Nassr na Ureno. Ronaldo kwa sasa ndiye mfungaji bora wa Ligi Kuu Saudi Arabia, Saudi Pro League. Namba zake ni neno la kuvutia sana. Ronaldo amefunga mabao 20 na kutoa asisti 10 katika mechi 22 alizocheza kwenye mashindano yote akiwa na Al-Nassr hadi sasa msimu huu.

## Nukuu

"Mchezo wa ajabu wa soka, moja ya makali ambayo nimeshuhudia kwa miaka 20 kwenye ligi hii. Kwa muda mrefu tulikuwa juu, katika dakika 20 za mwisho tulitaka zaidi, lakini sare ni matokeo ya haki. "Tulidhamiria kushambulia na kuwasababishia matatizo. Ni timu inayosababisha shida - wako wima na wa moja kwa moja. Ni bora zaidi duniani kufanya hivyo," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, baada ya sare ya bao 1-1 juzi dhidi ya Liverpool.**



"Ni aibu kwa Man Utd. Wamefunga mabao 18 msimu huu, ni Sheffield United pekee iliyofunga machache zaidi yake. Erik Ten Hag anasema 'tunapaswa kushikamana na mpango' lakini sijapata fununu ni mpango gani huo. Kuna kitu kibaya sana," **Mshambuliaji wa zamani wa Uingereza, Alan Shearer, baada ya Man United kuchezea kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya West Ham United juzi.**



"Nadhani kama wataleta mshambuliaji, Arsenal itatwaa ubingwa wa Ligi Kuu England," **Mchambuzi Lee Hendrie anaamini ni mshambuliaji tu anahitajika Arsenal kabla ya kutwaa ubingwa msimu huu.**



# MAKIPA 10 BORA WA WAKATI WOTE

**LONDON,** England

MAGOLIKIPA 10 bora wa wakati wote wameorodheshwa na mtandao wa ChatGPT, kwenye orodha hiyo yupo nyota wa zamani wa Manchester United, Peter Schmeichel na gwiji wa Real Madrid, Iker Casillas.

**Mara nyingi makipa wamekuwa ndio nyota wasio na sifa katika historia ya soka licha ya kuwa muhimu kwa mafanikio ya timu.**

Iwe ni ushujaa wa penalti, uokoaji wa dakika za mwisho, au usambazaji wa mipira hauwezi kupuuzwa.

Makala haya inawaangalia magolikipa 10 bora wa wakati wote.

**10. Sepp Maier**

Nyota huyu wa Ujerumani aliitwa "Die Katze" (paka) katika nchi yake. Alicheza mechi 217 bila kuruhusu bao kati ya 706 kwenye mashindano yote, akishinda Kombe la Dunia na Ulaya mara mbili wakati wa uchezaji wake.

**9. Edwin Van der Sar**

Mholanzi huyo ndiye kipa pekee aliyeshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na klabu mbili tofauti, Ajax mwaka 1995 na Manchester United mwaka 2008. Alikuwa nguzo ya kweli akicheza mechi 230 bila kuruhusu bao kati ya 821.

**8. Iker Casillas**

Casillas alikuwa na kazi nzuri ya kushinda Kombe la Dunia na Euro mara mbili akiwa na Hispania. Alicheza mechi 330 bila kuruhusu bao kati ya 881 katika michuano yote.

**7. Manuel Neuer**

Nyota huyu wa Bayern Munich bado anaendelea vema akiwa na umri wa miaka 37. Ameandikisha mechi 344 bila kuruhusu bao kati ya 752, akishinda Kombe la Dunia akiwa na Ujerumani na mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.




GIANLUIGI BUFFON

**6. Peter Schmeiche**

Schmeichel alicheza mechi 98 bila kuruhusu bao kati ya mechi 566 katika mashindano yote, na aliisaidia Manchester United kushinda mataji matatu mwaka 1999.

**5. Oliver Kahn**

Kabla ya wakati wa Neuer, Kahn alikuwa kipa mkuu wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ujerumani. Alicheza mechi 248 bila kuruhusu bao kati ya 785.

**4. Gianluigi Buffon**

Buffon alistaafu soka baada ya kucheza kwa muda wa miaka 28 akiwa na umri wa miaka 45, Agosti mwaka huu. Gwiji huyo wa Juventus alishinda Kombe la Dunia akiwa na Italia na kufikisha mechi 120 bila kuruhusu bao katika mechi 975 kwenye michuano yote.

**3. Gordon Banks**

Banks alikuwa na wakati mzuri wa mafanikio wakati wa uchezaji wake akishinda Kombe la Dunia akiwa na England mwaka 1966 kabla ya kufanya 'save ya karne' miaka minne baadaye akiokoa mpira wa kichwa wa Pele. Alicheza mechi 55 bila kuruhusu bao kati ya 322 katika mashindano yote.

**2. Dino Zoff**

Zoff aliiongoza Italia kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka 1982 akiwa na umri wa miaka 40, na kuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kushinda kombe hilo. Pia alikuwa kipa mahiri, akicheza mechi 231 bila kuruhusu bao kati ya 837,

**1. Lev Yashin**

Yashin anachukuliwa kuwa kipa bora zaidi wa wakati wote. Akitajwa na wengi kama "Buibui Mweusi", alicheza mechi 178 bila kuruhusu bao kati ya 358 katika mashindano yote.

Mchango wake kwenye mchezo huo ilikuwa mkubwa zaidi na jina lake lilipewa heshima ya kuitwa kwenye tuzo ya makipa bora wa dunia.




PETER SCHMEICHE

**JE, WAJUA?**



MANCHESTER United wamepoteza mechi 13 kati ya 26 zilizopita katika mashindano yote msimu huu, hii ni idadi kubwa ya vipigo kama walivyorekodi katika michezo 62 ya mashindano yote msimu uliopita. Lakini katika msimu wa Ligi Kuu, mara pekee wameweza kufunga mabao chini ya 18 baada ya mechi 18 za kwanza za ligi ni msimu wa 1973-74 (mabao 15), 1972-73 (mabao 16) na 1893-94 (mabao 15).



# Taasisi za umma zatakiwa kuwasilisha mipango utekelezaji miradi vijiji, kata

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Singida mjini kimezitaka taasisi za umma kuwasilisha mipango yao ya utekekezaji wa miradi kwenye vijiji na kata wananchi waifahamu ili kupunguza maswali ya mara kwa mara.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Singida Mjini, Lucia Mwiru, alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya uliokaa kujadili utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2020/2025.

Alisema wananchi wanahaki ya kujua kinachoendelea katika maeneo yao na kwamba wakijulishwa mapema kutasaidia kupunguza migogoro wakati wa utekelezaji wa mradi.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA), Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD).

Alisema taasisi hizo zinawajibika kueleza kwa wananchi miradi inayotekelezwa kwa kuwa miradi yao wanayoitekeleza inagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya jamii.

Alisema mipango hiyo ikiwasilishwa katika kata na vijiji itawawezesha wajumbe wa mkutano huo ambao ni wenyeviti na makatibu wa siasa katika kata kuisemea vyema kwa wananchi na kuondoa mashaka ama vikwazo wakati wa utekelezaji.

Nao wajumbe wa mkutano huo walipongeza kazi nzuri zinazofanya na Mkuu wa Wilaya ya Singida Mhandisi Paskasi Muragili katika kuongoza, kushauri na kusimamia kwa umakini shughuli za maendeleo katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

"Mkuu wetu wa wilaya anastahili pongezi kwani anajituma, anashauri na kusimamia vizuri shughuli za maendeleo katika wilaya yake yenye halmashauri mbili bila kuchoka, si jambo rahisi," alisema Mwiru.

Katika kuthamini mchango wake, Kamati ya Siasa ya Wilaya ilimpatia cheti na barua ya pongezi mkuu huyo wa Wilaya kwa mchango wake katika shughuli za maendeleo, utii na uwajibikaji mahiri katika majukumu yake ya uongozi.

Pongezi hizo zilielekezwa pia kwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu, ambaye pia alitunukiwa cheti kutokana na usimamizi mzuri na kujituma kwake katika shughuli za maendeleo.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe naye alipewa barua ya pongezi kutokana na utekelezaji mzuri wa ilani ya CCM kwa kujituma na kuwa kiungo baina ya chama na serikali.

Kabla ya mkutano kuanza, wajumbe wa mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Singida Mjini, walipata nafasi ya kutembelea miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa katika Manispaa ya Singida.

Aidha, wajumbe hao walipongeza matumizi mazuri ya fedha za mapato ya ndani ambayo matunda yake yameonekana katika miradi mbalimbali ya maendeleo ukiwemo mradi mkubwa wa ujenzi wa kituo kipya cha Afya kata ya Mtipa.



Katibu wa Kampeni ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), Kanda ya Ziwa, Hashim Omary (kulia), akimkabidhi Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza, Omary Mtuwa, cheti cha pongezi kwa ushirikiano katika kampeni dhidi ya vitendo vya ukatili juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati yakemea wanaojisifia kutafuna fedha za serikali

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KAMATI ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashekhe ya Maadili, Amani na Haki za Binadamu kwa jamii ya madhehebu nchini, imekemea kundi baya linalojisifia kupiga fedha za serikali.

Aidha, kamati hiyo imesema kundi hilo ni la hatari na lisikubarike kwa kuwa linaweza kuwa chanzo cha kujenga tabaka kwa walichonacho na wasionacho.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Wiliam Mwamalanga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana.

Askofu Mwamalanga aliiomba serikali kwa mwaka wa 2024 wapigwe marufuku watu hao na wote wanaotajwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali (CAG) watangazwe hadharani ili kushusha moto unaoendelea kuwaka kwenye mioyo ya Watanzania walio wengi.

"Sisi kamati ya kitaifa ya mashekhe na maaskofu kwa pamoja na Watanzania tunalikemea kundi hilo baya lililoibuka ambalo linalojisifu kwa kupiga fedha za serikali kwa kweli hili halikubalika kwani linaweza kuligawa taifa," alisema.

Hata hivyo, kamati hiyo imepongeza serikali kwa kushiriki katika kuokoa waathirika wa maporomoko ya matope na magogo katika mji wa Kateshi mkoani Manyara bila kuangalia itikadi yoyote ya dini, kabila ,siasa na rangi.

"Tunazipongeza taasisi binafsi mashirika ya ndani na nje wakuu wa mikoa na wilaya na wananchi kwa kazi njema kwa wakati wote kwa kuwahudumia waathirika wote wa maafa hayo.

Pia tunampongeza Rais wetu kwa upendo wake ambao tumeuona kwa waathirika wa wilaya ya Hanang ambao walivamiwa na mafuriko mabaya ambayo hayajawahi kutokea tangu uhuru wa nchi upatikane," alisema.

Hata hivyo kamati hiyo imewaomba Watanzania wote bila kujali itikadi zao za kidini kuzitumia pia sikukuu za Krismas na mwaka mpya kuungana kwa pamoja kumwombea Rais na serikali.

Alisema sikukuu hizo zisitumike kwa kufanya vurugu na kuhatarisha maana halisi ya krismas na mwaka mpya, bali Watanzania washerehekee kwa amani na upendo.

# Dk. Tulia mgeni rasmi ibada ya mwaka mpya

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Akson, anatarajiwa kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika ibada ya mkesha mkuu wa mwaka mpya utakaofanyika uwanja wa Nyerere Squar Desemba 31, 2023 jijini Dodoma.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Fellowship of Churches (TFC), Dk. Godfrey Malasi, alisema hayo juzi jijini hapa, alipozungumzia na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya ibada hiyo.

Alisema Spika wa Bunge atamwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alikuwa awe mgeni rasmi kwenye ibada hiyo ya mkesha ambayo ufanyika kila mwisho wa mwaka Desemba 31.

Askofu Dk. Malasi alisema kuwa mkesha huo utafanyika kitaifa katika mkoa huo lakini kuna maeneo mengine yatakuwa wakifanya ibada kama hiyo.

Alisema miongoni mwa maeneo hayo kuwa ni Mkoa wa Dar es Salaam, Arusha, Singida, Iringa Zanzibar, Moshi na Dodoma.

"Na mpaka sasa maandalizi ya ibada hiyo ya mkesha kwa maeneo yote saba yamekamilika kwa asilimia 100, hii ni pamoja na kuwapata viongozi ambao watakuwa wageni rasmi kwenye mikesha hiyo,' alisema.

Alitaja baadhi ya viongozi watakaojumuika kwenye mikesha hiyo ni pamoja na Naibu Waziri Mkuu na Wazir wa Nishati Dk. Dotto Biteko ambaye atakuwa Dar es Salaam na Zanzibar atakuwapo Rais Dk. Hussen Ali Mwinyi.

Dk. Malasi, aliwataka Watanzania kuimarisha umoja amani na mshikamano kwa mustakabali mwema wa Taifa katika siku za usoni na kuepuka vurugu ambazo zaweza kusababisha migogoro katika jamii.

Alisema amani na utulivu vinatakiwa kupewa kipaumbele na Watanzania wakikataa kutumiwa vibaya na nchi itazidi kuwa imara katika nyanja zote.

Dk. Malasi ambaye ni mwanzilishi na mbeba maono ya mikesha hiyo tangu ilivyoanzishwa mwaka 1997, alisema kuwa Watanzania lazima wajivunie tunu hiyo ya amani na utulivu ambayo Mungu ametupatia.



# Polisi yatoa angalizo kwa wazazi sherehe za Krismasi, Mwaka Mpya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewatahadharisha wazazi na walezi watakaokwenda na watoto kwenye maeneo ya mapumziko wakati wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya ikiwamo kwenye fukwe mbalimbali za Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Kyela kuwa makini ili kuepuka maafa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga alitoa tahadhari hiyo juzi alipozungumza na wandishi wa Habari kuhusu namna ambavyo jeshi hilo limejipanga kuimarisha usalama.

Alisema wamiliki wa fukwe na maeneo yote ya mapumziko kuweka waangalizi maalumu watakaosaidia kuzuia ajali ambazo zinaweza kutokea kwenye maeneo hayo.

Alisema jeshi hilo limejipanga kuhakikisha sherehe hizo zinafanyika kwa amani na utulivu ikiwamo ibada ambapo alisema zitakuwa zinafanyika doria kwenye maeneo mbalimbali.

"Tutashirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama za Makanisa katika kuimarisha ulinzi wakati wa ibada na misa hasa zile za mkesha, lakini pia tutakuwa tunafanya doria kwenye maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu," alisema Kamanda Kuzaga.

Aidha aliwataka madereva wote wa vyombo vya moto mkoani humo kuendelea kuwa makini wawapo barabarani ili kuepusha ajali ambazo zinaweza kusababisha madhara kwao, kwa watumiaji wengine wa barabara pamoja na vyombo vyao vya usafiri.

Alisema kwenye miteremko ya Mlima Shamwengo na Mbalizi jeshi hilo litaendelea kusimamia magari kupita kwa awamu ili kuepusha ajali na akawataka madereva kuendelea kuwa wavumilivu.

# Mvua yaua mmoja, 198 wakosa makazi Mbarali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MTU mmoja amefariki dunia na wengine 198 kukosa makazi katika Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya baada ya mvua iliyoambatana na upepo mkali kubomoa nyumba 44 kwenye maeneo tofauti ya kata sita.

Mratibu wa Maafa wa Wilaya ya Mbarali, Lihuwi Ngonyani, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, kukagua madhara yaliyosababishwa na mvua hiyo na kukabidhi misaada.

Ngonyani alimtaja mtu aliyefariki kuwa ni John Ngomban mkazi wa Kijiji cha Luhanga baada ya kuangukiwa na nyumba wakati mvua hiyo ikinyesha.

Alizitaja kata zilizoathiriwa na mvua hiyo kuwa ni Igurusi, Chimala, Ruiwa, Mahongole, Mawindi na Luhanga ambapo madhara yalitofautiana kutoka eneo moja hadi lingine.

Alisema mvua hiyo ilileta madhara makubwa kwa baadhi ya kata kwa sababu ilinyesha mchana, muda ambao watu wengi walikuwa wapo kwenye shughuli zao za kila siku. "Bahati nzuri ni kwamba watu wengi walijiokoa kwa kukimbia maana ilikuwa mchana wakati mvua hii inanyesha, bahati mbaya ni kwamba mzee huyo mmoja ndiye alifariki na hakukuwa na majeruhi ila nyumba nyingi zimeharibika kabisa," alisema Ngonyani.

Mmoja wa wananchi hao, Merina Asumwisye, alisema wakati upepo unavuma alikuwa ameshatoka nyumbani kwenda kwenye shughuli zake za kilimo huku akiwa amemwacha kijana wake wa kiume akiwa amelala ndani.

Alisema wakati kijana huyo amelala ndani alisikia kelele kwa majirani ndipo akatoka kwenda kuangalia kilichokuwa kimetokea na ndipo akakuta nyumba za majirani zinaezuliwa na upepo na zingine zinaanguka.

Alisema baada ya kijana huyo kutoka kwenye nyumba yao ndipo akakuta na yenyewe inaezuliwa mabati na kuta zote zikadondoka na kuharibu vitu vyote vilivyokuwamo ndani.

"Namshukuru Mungu kwa kumwokoa mwanangu, yawezekana asingesikia kelele kwa majirani asingetoka maana alipotoka ndipo nyumba ilianza kuanguka, kwa sasa tunaishi kwa majirani zetu ambao nyumba zao zilipona," alisema Merina.

Mchungaji wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Dankeni Mwangengele, alisema alipigiwa simu na mmoja wa waumini wake akieleza kuwa kanisa limebomoka.

Alisema alipokwenda kuangalia alikuta kweli kanisa lote limeanguka pamoja na baadhi ya nyumba za jirani na ndipo wakashirikiana kutoa baadhi ya vitu ambavyo vilikuwa havijaharibika.

Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Bahati Ndingo aliwataka wananchi ambao nyumba zao zilipona kuendelea kuwahifadhi wenzao ambao waliathirika na mvua hiyo mpaka nyumba zao zitakapokuwa zimerejea katika hali ya kawaida.

Vilevile aliwataka wananchi kuendelea kuwa makini kwa maelezo kuwa mwaka huu Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imetangaza kuwa kutakuwa na mvua nyingi na hivyo kuna uwezekano madhara yakaendelea kutokea.

Naibu Waziri Nderiananga mbali na kuwapa pole wananchi hao, alikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa waathirika ikiwemo vifaa vya ujenzi, vifaa vya kulalia pamoja na vyakula.

"Pamoja na changamoto iliyotokea kule Hanang ambayo tumeendelea kushughulikia, lakini serikali imetoa zaidi ya Sh. milioni 23 kwa ajili ya misaada kwa wananchi wa kata hizi sita waliopata maafa, kuna magodoro 100, mifuko 200 ya saruji pamoja na mabati 500," alisema Naibu Waziri Ummy.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mkuu wa Wilaya ya Mbaye, Beno Malisa aliishukuru serikali na kuahidi kugawa misada hiyo kwa walengwa wote wa maafa hayo.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa Mbunge wa Mbarali, Bahati Ndingo, kuhusu maafa yaliyosababishwa na mvua iliyoambatana na upepo, kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Bil. 18/- kujenga kampasi ya UDOM mkoani Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imetenga Sh. bilioni 18 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kampasi mpya ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) katika Halmashauri ya Mji Njombe kwa lengo la kusogeza huduma ya elimu kwa wananchi.

Akitoa taarifa kwenye Kikao cha Ushauri cha mkoa huo (RCC) mwishoni mwa wiki, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lughano Kusiluka, alisema kampasi hiyo itakuwa ya kwanza ya chuo hicho katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Prof. Kusiluka alisema kutokana na vigezo uongozi wa chuo hicho umependekeza makao makuu ya kampasi hiyo yajengwe katika eneo lililotengwa Njombe mjini lililopo karibu na Shule ya Sekondari Njombe (NJOSS). Alisema eneo hilo lina ukubwa wa ekari 110 na kwamba wanakusudia pia kulitumia eneo la Ihalula lenye ukubwa wa ekari 320 kwa ajili ya mafunzo.

"Sisi tunapendekeza kwa mamlaka na uongozi wa mkoa wa Njombe kwamba makao makuu ya kampasi ya chuo kikuu cha Dodoma mkoa wa Njombe iwe katika eneo hili lililopo mjini," alisema Prof. Kusiluka.

Aidha alishauri eneo lililopo katika kijiji cha Ihalula lenye ekari 320 pia itolewe kwa ajili ya ujenzi wa kampasi kwa sababu programu wanategemea kuanzisha program zinazoakisi shughuli za kiuchumi na kijamii za mkoa huo na jirani,

Aidha Prof. Lughano alisema chuo kikuu cha Dodoma kitakachojengwa Njombe kitachukua kozi za ufugaji, kilimo, Mawasiliano na teknolojia mbalimbali.

Mratibu Msaidizi wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Uchumi, Dk.Evaristo Mtitu, alisema mradi huo ni wa miaka sita ambapo matarajio ni kuwa ifikapo mwaka 2026 chuo kiweze kuanza kufanya kazi.

"Tunaomba ushirikiano wa wananchi ili UDOM wasikwame kwa kuwa mradi huu ni wa miaka sita 2021 - 2026 chuo kinatakiwa kiwe kimesimama na kinafanya kazi," alisema Mtitu.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alisema kuwa wananchi wa mkoa huo wamekuwa na shauku ya muda mrefu kuona unakuwa na Chuo Kikuu na kumshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kujali maombi ya wananchi wa Njombe.

Pia Mtaka, aliwataka wananchi kutumia fursa mbalimbali katika uwekezaji ambao utaleta ushindani katika suala zima la kiuchumi. Naye Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, Deo Mwanyika, alisema ujuzi utakaozalishwa katika mkoa huo kupitia chuo hicho utaleta mageuzi kiuchumi kwa wananchi wa mkoa huo.

"Kwa hiyo niwaombe focus kubwa kwenye kozi zote mwisho wa siku kwetu sisi msisahau biashara na ujasiriamali," alisema Mwanyika.



# Wananchi waagizwa kuitunza miundombinu ya barabara

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amewataka wananchi kuilinda na kuitunza miundombinu ya barabara ili idumu kwa muda mrefu.

Hamza aliyasema hayo jana wakati akizindua Barabara ya Dunga-Zuze iliopo Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja na kuwaeleza masheha kuzuwia ujenzi holela unaofanywa na watu wasiozingatia sheria.

Waziri huyo aliwakumbusha wananchi kuzingatia na kufuata sheria hasa za hifadhi ya barabara ikiwamo kuepuka kujenga nyumba karibu na hifadhi hiyo.

Alisema wapo wananchi ambao huibuka na kujenga nyumba zao katika maeneo ya hifadhi ya barabara jambo linalosababisha usumbufu wakati serikali inapotaka kutanua barabara hizo.

Hamza alimpongeza Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa hatua anazozichukua katika uimarishaji wa miundombinu na huduma za jamii Zanzibar jambo linaloifanya Zanzibar kupiga hatua za kimaendeleo.

"Kwa kweli niwambie Rais Dk. Mwinyi katika kipindi chake hiki ameimarisha sana miundombinu kiasi ambacho inazishinda nchi nyingi barani Afrika," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kati, Sadifa Juma Khamis, aliipongeza Wizara ya Ujenzi kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa barabara zilizojengwa katika Mkoa wa Kusini.

Sadifa alimtaka Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi kuangalia uwezekano wa kuzisaidia kambi mbalimbali kwa kuzingiza barabara zao katika mpango maalum wa ujenzi kutokana na umuhimu wao katika kuimarisha ulinzi na usalama.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Khadija Khamis Rajab alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kutekeleza mipango ya maendeleo kwa maslahi ya wananchi na nchi kwa ujumla.

Khadija alisema, Wizara ya Ujenzi inaendelea na usimamizi wa ujenzi wa barabara za mijini pamoja na barabara za ndani ambapo muda wa utekelezaji wa barabara hizo za ndani ni miezi 40 na mara baada ya kukamilika zitakua chini ya uwangalizi kwa kipindi cha siku360 .



Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Salum Khamis Rashid (kulia), akikabidhi msaada wa chakula katika kituo cha yatima cha Assalam Orphan Centre, uliotolewa na Mamlaka ya Mafunzo na Amali juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda cha kusarifu dagaa kuiinua Zanzibar kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR inatarajia kuingiza mamilioni ya fedha baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa kinachoendelea kujengwa Kama, Wilaya ya Magharib A Unguja, chenye uwezo wa kuzalisha tani 20 kwa siku zenye thamani ya ziadi ya milioni 200.

Akizungumza jana katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi wa kiwanda hicho, Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Suleiman Aboud Jumbe, alisema kiwanda hicho kitakapokamilika kitakuwa cha aina yake katika ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki.

Alisema dagaa ni moja wapo ya mazao makuu ya kimkakati visiwani humo katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini na kuliinua zao hilo kupitia ushindani wa kisasa kwa ubora katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Katibu mkuu huyo alisema chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, uzalishaji wa dagaa umekuwa kutoka tani 2,405 zenye thamani ya Sh. bilioni 10.33 hadi tani 21,827 za Sh. bilioni 89.31.

Alisema pia usafirishaji wa dagaa umeongezeka kutoka tani 3,579 zenye thamani ya Sh. bilioni 12.31 mwaka 2020 hadi kufikia wastani wa tani 9,000 zenye thamani ya Sh. milioni 35 kwa mwaka huu wa 2023.

Aidha, alisema mafanikio ya sekta ya dagaa yamechochea kuongeza kwa uzalishaji wa jumla wa sekta ya uvuvi wa samaki kutoka tani 38,107 kwa mwaka 2020 hadi tani 80,085 zenye thamani ya Sh. bilioni 569.08 kwa mwaka huu.

"Ongezeko hilo ni ushahidi mkubwa wa kihistori na limewezesha wavuvi kupata ajira na kuinua hali zao za maisha. Takwimu za hivi karibuni zinaonesha kuendelea kukua kwa kasi kubwa kwa sekta ya uvuvi nchini kwa kiwango cha asilimia tisa kwa mwaka," alisema Jumbe.

Katibu mkuu huyo alisema mchango wa sekta ya uvuvi katika uchumi wa buluu umeongezeka kufikia wastani wa asilima 17.40 ambapo hayo ni mafanikio makubwa na uwepo wa kiwanda cha kukausha dagaa utachocheza zaidi ongezeko la kipato cha uchakataji wa samaki kutoka wastani wa sasa wa Sh. 435,300 lakini kuongeza kipato cha wajasiriamali wa samaki kutoka wastani wa sasa wa Sh. 742,500.

Alisema kiwanda hicho kitakapomalizika kitaongeza ajira kwa wananchi na takwimu za sasa zinaonesha asilimia 21 ya ajira za wananchi wote wa Zanzibar zinatokana na sekta zote za uchumi wa buluu na sensa ya wisho ya uvuvi ya mwaka 2020 Zanzibar inawavuvi 88,000.

Naye Mkurugenzi wa kampuni ya uvuvi Zanzibar (ZAFICO), Amiri Haidar Mshenga, alisema mradi huo wa kujenga miundombinu ya dagaa ni miongoni mwa utekelezaji wa ahadi ya Rais Dk. Mwinyi ambae aliwaahidi wananchi wajasiriamali wa usarifu wa dagaa sambamba na utekelezaji ilani ya uchaguzi wa CCM.

Alisema Zanzibar inawastani wa wajasiriamali 16,000 wa dagaa ambapo Unguja wapo 14,000 na 12,000 Pemba na jumla maeneo matatu yametengwa kwa ajili ya mradi wa usarifu wa dagaa ikiwamo Kama, Fungu refu na Ndagoni.

Alisema mradi huu unatarajia kutumia Sh. milioni 23 ambazo zimejumuisha ujenzi wa viwanda viwili vya kusarifu dagaa, ujenzi wa majengo ya kuoshea dagaa, majengo ya kuchemshia dagaa, jengo la mtambo baridi kwa ajili ya kuhifadhia dagaa na mtambo wa kuzalisha barafu na jengo la biashara.

"Hadi kukamilika kwa kiwanda hiki sisi ZAFICO tutaweka chanja 5000 za kuanikia dagaa na mradi huo kwa awamu ya kwanza utakamilika Februari mwakani na unatarajiwa kuajiri wajasiriamali zaidi ya 10,000 wakiwamo wavuvi na wafanyakazi wa sekta ya dagaa," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Suleiman Said, alisema Zanzibar ina utajiri mkubwa wa uvuvi hivyo bahari ikitumiwa vizuri italeta maendeleo makubwa kupitia fursa zilizomo baharini na ukanda wa pwani.

Alisema uvuvi ni muhimu kwa maendeleo ya jamii katika nchi na ili sekta ya uvuvi ilete tija hakuna budi kutumia teknolojia za kisasa na ushirikishwaji wa sekta binafsi, ndio maana serikali inahamasisha wananchi kuendelea nau vuvi endelevu usioharibu mazingira ya bahari.

Alikemea uvuvi haramu na kuvielekeza vyombo husika kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti tabia hiyo isiendelee ili kuepusha madhara kwa ikolojia ya bahari na walaji wa kitoweo hicho.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa wananchi wa Zanzibar wanatumia samaki kwa wastani wa kilo 22 kwa mtu mmoja kwa mwaka, kiasi hicho ni kikubwa kulinganisha na wastani wa matumizi ya kiwango cha dunia ambacho ni kilo 20.5 kwa mtu mmoja kwa mwaka.

Aidha aliwataka wananchi kuongeza kiwango cha matumizi ya chakula kinachozalishwa baharini ikiwemo dagaa kwa kuimarisha afya ya lishe kwa wananchi.

Uwekaji wa jiwe hilo la msingi wa kiwanda hicho cha kusarifu dagaa ni miongoni mwa shamrashara za Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# Power Energy kuleta suluhu ya changamoto ya umeme

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar imetiliana saini ushirikiano wa makubaliano na kampuni ya Powgex Energy ya Australia kwa ajili ya utafiti wa uzalishaji wa umeme wa upepo megawati 450 zitakazomaliza changamoto ya umeme kisiwani humo.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika utiaji saini huo ulifanyika katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Shaibu Kaduara, alisema kati ya Megawati hizo 450, 300 zitazalishwa Unguja na 150 Pemba na utakuwa chini ya bahari.

Alisema serikali ya Zanzibar hairuhusu makubaliano kuchukua muda mrefu bila ya utendaji hivyo aliiagiza kampuni hiyo kuharakisha maandalizi ya utafiti huo.

Alipongeza kampuni hiyo kuwekeza Zanzibar na kuzikaribisha kampuni nyingine zenye nia kama hiyo kujitokeza na serikali imeweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuwapokea wawekezaji.

"Ushirikiano huu uende kuleta tija katika pande zote mbili lakini pia yajenge udugu na urafiki zaidi ili kila upande ufikie malengo yake," alisema Kaduara.

Mkurugenzi wa mradi huo kutoka kampuni ya Powgex Energy, Charles Lwanda, alisema mazingira mazuri na wezeshi yaliyowekwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio imevutia kampuni hiyo ya kimataifa yenye uzoefu katika uzalishaji wa umeme kuwekeza kisiwani humo.

Alisema mradi huo unaokadiriwa kufikia dola za Marekani 1.2 bilioni utaisaidia Zanzibar sio tu kufikia malengo yake, pia kuwa na kiwango cha ziada cha mahitaji.

Alisema makubalino hayo ni kwa ajili ya kufanya utafiti na kuja matokeo ya upembuzi yakinifu na kuwa na mpango wa mradi kuanza uzalishaji wa kiwango hicho cha umeme. "Hii itahusisha upembuzi yakinifu na kushirikisha ujenzi wa miundombinu kwa lengo la kuzalisha na kusimika mitambo ya kuzalisha umeme Zanzibar. Pia mradi huu utasaidia kutunza mazingira kwasababu miundombinu yake inawekwa baharini na pwani," alisema.

Alisema umeme huo utazingatia matumizi ya umeme wa viwandani na kupeleka nje kupitia teknolojia za kebo za baharini.

# Bil. 5.3/- zahitajika kukarabati miundombinu wilayani Kilosa

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, amesema zaidi ya Sh. bilioni 5.3 zinahitajika kurudisha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko wilayani hapa.

Miundombinu hiyo ni iliyoharibiwa na mafuriko yaliyotokea mwanzoni mwa Desemba mwaka huu katika maeneo mbalimbali wilayani hapa.

Alitoa taarifa hiyo kwa Mkuu wa Mkoa Morogoro, Adam Malima, wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa maagizo yake aliyoyatoa kwa watendaji wa serikali ya mkoani hapa ya urejeshaji wa miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko hayo.

Shaka alisema mafuriko hayo yalisababisha vifo vya watu watatu na kuathiri kaya 1,470, kubomoa nyumba 316 na nyingine 1,042 kuzingirwa na maji pamoja na uharibifu wa ekari 303 za mashamba.

Alisema waathirika waliokosa makazi hadi sasa wamehifadhiwa katika shule mbili zilizotengwa wakati mahitaji yanayohitajika ni vyandarua, chakula, magodoro, dawa za kutibu maji, sabuni, mavazi, na vifaa vya shule kwa watoto waliopoteza vifaa vyao.

Alisema mafuriko hayo yalisababisha madaraja matatu kukatika na kusababisha kukosekana kwa mawasiliano kati ya Mji wa Kilosa na maeneo mengine.

"Mpaka sasa tathmini iliyofanyika kuhusiana na mafuriko haya Sh. bilioni 5.3 zinahitajika ili kurudisha katika hali yake miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko," alisema Shaka.

Naye Mbunge wa Kilosa, Profesa Paramagamba Kabudi, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh. milioni 900 zilizotumika kujenga mifereji ya maji ili kuboresha miundombinu wilayani hapa.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Malima akizungumza na watendaji wa wilaya hiyo alitaka hatua zichukuliwe ikiwamo kuwataka wananchi wanaoishi mabonde na mikondo ya maji waondoke kwa kuwapatia viwanja maeneo salama, ili kuwaepusha na kupatwa mafuriko ya mara kwa mara.

Malima, alisema Wilaya ya Kilosa imekuwa na historia ya kukumbwa na mafuriko ya mara kwa mara yanayosababisha uharibifu wa miundombinu, mali za wananchi na hata kusababisha vifo.

Alisema siyo jambo jema kuendelea kulalamika kila yanapotokea mafuriko kwani hivi sasa zinahitajika hatua mbalimbali zichukuliwe ikiwamo kufanyika kwa utafiti zaidi ili kudhibiti mafuriko ya mara kwa mara.

Alitaja moja na mikakati inayopaswa kuchukuliwa ni kuvuna maji kwa kuchimba mabwawa ambayo yatakusanya maji yatakayotumika katika shughuli nyingine za kibinadamu zikiwamo za umwagiliaji na matumizi mengine ya kawaida kipindi cha kiangazi.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maabara ya Veterinari nchini (TVLA), Dk. Stella Bitanyi, akisisitiza jambo wakati akifungua mafunzo ya wazalishaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Kulia ni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo, Rogers Shengoto na Mkurugenzi wa Huduma na Uchunguzi wa wakala huo, Dk. Zacharia Makondo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazalishaji, wauzaji vyakula mifugo wapigwa msasa

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi chini ya Taasisi ya Wakala ya Maabara ya Veterinari (TVLA), imewapa mafunzo ya siku moja wazalishaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo kutoka mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Akifungua mafunzo hayo, Mtendaji Mkuu wa Wakala hiyo Dk. Stella Bitanyi, amesema hatua hiyo imetokana na malalamiko ambayo serikali imeyapokea kutoka kwa wafugaji wa kuku ambao wanalalamikia udumavu wa kuku unaohusishwa na ubora hafifu wa vyakula vya mifugo sokoni.

"Tumeona tuwaite na kuwapa mafunzo haya kwa sababu hatutaki kurudi kwenye kile kipindi ambacho wafugaji walikuwa wanaagiza vyakula vya mifugo kutoka nje ya nchi kwa sababu kufanya hivyo ni kuua viwanda vyetu vya ndani," alisema Dk. Bitanyi.

Aidha, amesisitiza taasisi yake itaendelea kushirikiana kwa ukaribu na wazalishaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kukagua utekelezaji wa waliyoelekezana kwenye mafunzo hayo kazi itakayofanywa na kikosi kazi kutoka kwenye taasisi hiyo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Idara yake ya nyanda za malisho na vyakula vya mifugo na wakaguzi kutoka kwenye mikoa na wilaya zote nchini.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji Malisho na Rasilimali za vyakula vya mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Rogers Shengoto, amesema wizara yake imetumia mafunzo hayo kuwasisitiza wadau wote wa tasnia ya vyakula vya mifugo kuhakikisha wanasajili shughuli zao kwa mujibu wa Sheria ya Maeneo ya Malisho sura namba 180 pamoja na kanuni zake.

"Lakini pia msitumie nafaka au rasilimali za vyakula zisizofaa kwa matumizi ya binadamu kutengenezea vyakula vya mifugo kwa sababu mnyama akiathirika humuathiri pia mlaji anayekula nyama ile," alisema Shengoto.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo mzalishaji wa vyakula vya mifugo, Mohammed Mshana, ameishukuru serikali kwa kuwawezesha mafunzo hayo na kushauri iwe endelevu ili waweze kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa tija.

Akielezea namna mafunzo hayo yalivyomuwezesha kufahamu matumizi sahihi ya chanjo za mifugo, mmoja wa washiriki mfugaji kutoka Wilaya ya Kigamboni, Albina John, amesema kwa sasa anatarajia kuanza kutibu mifugo yake kwa wakati tofauti na ilivyokuwa hapo awali na chanjo alizokuwa akinunua kutoka nje ya nchi zilikuwa hazimfikii kwa wakati.

Mafunzo hayo yamefanyika ikiwa ni wiki chache tangu kufanyika kwa operesheni maalum ya ukaguzi wa viwanda na maduka yanayouza vyakula vya mifugo ambayo iliendeshwa na Wakala ya Maabara ya Veterinari nchini (TVLA) na kubaini dosari mbalimbali kwa wadau hao wa ufugaji nchini.

## Magereza yaboresha mitaala urekebishaji tabia wafungwa

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

JESHI la Magereza limeanza uboreshaji wa mitaala ya urekebishaji wafungwa ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Mpango huo umelenga kuboresha baadhi ya maeneo yaliyokuwa na upungufu ambayo yanachangia kwa namna moja ama nyingine wahalifu kurudia makosa yao wanapokuwa uraiani.

Kamishna Jenerali wa Jeshi hilo, Ramadhani Nyamka, alisema hayo mkoani hapa wakati akizindua kazi ya uandaaji mitaala ya urekebishaji tabia kwa wafungwa kuanzia ngazi ya astashahada na shahada.

Alisema mitaala hiyo mipya itatumika kufundishia maofisa wa Jeshi la Magereza na askari kwenye vituo vyake waweze kwenda kutoa mafunzo yanayostahiki ya urekebu kwa wafungwa magerezani.

"Tulipewa maagizo na Rais Samia kuwa Jeshi la Magereza lihakikishe taratibu au programu za urekebishaji kwa wahalifu zinafanyika kwa kiwango stahiki na kinachokubalika," alisema Kamishna Jenerali Nyamka.

Nyamka alisema hata mapendekezo ya Tume ya Rais aliyoiunda kwa ajili ya maboresho ya vyombo vya haki jinai, moja ya mapendekezo yake yaliitaka Jeshi la Magereza liboreshe mitaala yake na lengo nikuwa kuwa na programu za urekebishaji.

Alisema mitaala hiyo itaweza kuwarekebisha wafungwa wanaoingia gerezani, wamalizapo vifungo vyao na kurudi uraiani kuijunga na Watanzania wengine katika shughuli za ujenzi wa uchumi wa taifa.

Kamishna Nyamka alisema kazi ya urekebishaji wahalifu ni ya kitaalamu, inahitaji miongozo na mitaala inayoakisi hali ya sasa na inayoendana na wakati.

Alisema mapitio ya mitaala, mafunzo sahihi kwa maofisa wa Jeshi la Magereza na askari katika tasnia ya urekebu yanatakiwa kupewa uzito unaostahili ndani ya jeshi hilo.

Kamishna Jenerali Nyamka alisema licha ya maboresho ya mitaala, jamii ina jukumu kubwa la kuwasaidia wafungwa wanaomaliza vifungo vyao ambao tayari wanakuwa na ujuzi ili waweze kujitegemea kiuchumi na siyo kuwanyanyapaa.

"Wakati mwingine mfungwa anapotoka gerezani kwa kutumia programu za urekebu gerezani amekuwa na taaluma ama ujuzi ambao alipoingia gerezani hakuwa nao, anapotoka ni fundi seremala mzuri, hivyo jamii iwe na utayari kuwasaidia," alisema.

Alishauri jamii iwasaidie watu hao kwa kuwapa vitendea kazi ambayo iyakuwa ni njia bora ya kumtengenezea mazingira ya kuendeleza ujuzi wake na kuweza kudumu maisha ya kila siku na kufanya tatizo la urudiaji wa makosa ufumbuzi wa kudumu.

Kaimu Meneja wa Ukuzaji Mitaala, Utafiti na Upembuzi Yakinifu kwa Soko wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Magreth Shawa, alipongeza Jeshi la Magereza kwa kufuata taratibu na miongozo iliyowekwa na baraza.

HABARI KIMATAIFA

# Cameron ainyooshea kidole Iran

**LONDON,** UINGEREZA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Uingereza, David Cameron, amesema kuwa nchi yake haitavumilia shughuli za Iran, ambazo alizitaja kuwa za uovu katika nchi yake na Mashariki ya Kati.

Cameron alithibitisha katika mahojiano na gazeti la Uingereza la 'The Sunday Telegraph' lililochapishwa jana kwamba Uingereza itaimarisha ushirikiano wake na washirika ili kuendeleza hatua za dhidi ya Iran.

Pia aliishutumu Iran kwa kusaidia mawakala wake wa Hamas, Houthi, na Hezbollah kuyumbisha utulivu wa kimataifa, akisema kuwa inatoa ndege zisizo na rubani, makombora na ujasusi wa kimbinu.

"Ujumbe wa onyo la wazi lazima upelekwe kwa Iran kutovumilia mashambulizi ya Houthi dhidi ya meli za kibiashara katika Bahari Nyekundu," alisema.

Ilielezwa kuwa tangu katikati ya Novemba, mwaka huu kundi la Houthi nchini Yemen limeanzisha mfululizo wa mashambulizi dhidi ya meli za kibiashara zinazovuka Bab al-Mandab.

Kundi hilo lilisema kuwa lilikuwa likilenga meli za Israel, kujibu kile walichokitaja kuwa mauaji ya Israel katika Ukanda wa Gaza na kuzingirwa kwake.

Uingereza inashiriki katika muungano mpya wa kimataifa, unaotambulika kama'Guardian of Prosperity' unaoongozwa na Marekani, kulinda harakati za biashara katika Bahari Nyekundu dhidi ya mashambulizi ya Houthi nchini Yemen.

Pia ilitangaza vikwazo vipya vinavyolenga wafanya maamuzi wa Iran na wale wanaotekeleza amri zake, akiwemo Ismail Qaani, kamanda wa Kikosi cha Quds cha Walinzi wa Mapinduzi ya Iran.

Cameron alipoulizwa kama London ilikuwa tayari kuweka hatua zaidi, alijibu kwamba suala hilo sio kwa ajili ya kujadiliwa kwa umma. **BBC**

# Wapinzani Kongo kufanya maandamano kupinga uchaguzi

**KINSHASA,** DRC

WAGOMBEA watano wa urais wa upinzani nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wamesema watafanya maandamano Desemba 27, mwaka huu mjini Kinshasa kupinga ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi mkuu uliomalizika.

Kwa mujibu wa Jean-Marc Kabunda, mwakilishi wa mgombea Martin Fayulu, wanasiasa hao waliwasilisha barua kwa gavana wa jiji la Kinshasa juzi.

Kabunda alisema barua hiyo inaelezea azma ya maandamano hayo ambayo ni ya kupinga ukiukwaji uliojitokeza wakati wa kupiga kura na kabla ya zoezi la kupiga kura na kuongezwa zoezi la kupiga kura kwa siku moja zaidi.

Pia alisema kasoro zilizotajwa kwenye barua hiyo ni za kutosha kuona kwamba Desemba 20, uchaguzi wa DRC ulikuwa wa udanganyifu.

Tume ya uchaguzi nchini humo, (CENI), ilikiri kuchelewa kuanza shughuli za kupiga kura Desemba 20 licha ya kwamba haikuwezekana kwa baadhi ya vituo kufunguliwa, huku ikikanusha madai ya kuongeza muda wa kupiga kura.

Rais wa CENI, Denis Kadima kwa mara nyingine alipinga ukosoaji wa upinzani na waangalizi huru kuwa uchaguzi huo uliorefushwa ulikuwa na vurugu na ulikosa uhalali.

Aidha, matokeo ya awali ya uchaguzi wa urais nchini humo yalianza kutolewa Ijumaa huku matokeo kamili ya awali ya uchaguzi huo yakiwa yanatarajiwa kutolewa Desemba 31.

Hata hivyo, Rais Felix Tshisekedi anayewania muhula wa pili madarakani alikabiliana na wagombea wengine 18 wa upinzani kwenye kinyang'anyiro cha urais.

Matokeo ya awali kutoka kwa maelfu ya wapiga kura wa jamii ya Wakongo walioko nje ya nchi yanaonyesha, Rais Felix Tshisekedi anaongoza dhidi ya wapinzani wake.

Matokeo hayo ni kutoka kwa raia wanaoishi Afrika Kusini, Ubelgiji, Ufaransa, Canada na Marekani.

**DW**



Wapalestina wakitafuta wanusura katika eneo lililotokea shambulio huko Ukanda wa Gaza juzi. **PICHA: REUTERS**

# Israel yaua 76 wa familia moja Gaza

## •Yaahidi kuendeleza vita hadi malengo yatimie

**GAZA,** PALESTINA

KWA mujibu wa shirika la habari la 'Associated Press' watu 76 kutoka familia moja wameuawa baada ya shambulizi la anga lililotekelezwa na Israel katika mji wa Gaza.

Ilielezwa kuwa shambulizi hilo lilitekelezwa juzi, huku Wizara ya Afya ya Hamas, ikibainisha kuwa mgomo wa Israel kwenye kambi ya wakimbizi ya Nusseirat pia ulisababisha vifo vya watu 18 usiku wa kuamkia Jumamosi.

Aidha, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, wakati akizungumza kwa njia ya simu na Rais wa Marekani, Joe Biden, aliweka wazi kwamba vita dhidi ya Gaza vitaendelea hadi malengo yao yote yatimie.

Wakati kauli hiyo ikitolewa, Wizara ya Afya ya Gaza ilieleza kuwa idadi ya vifo kutokana na operesheni za Israel katika ukanda huo imeongezeka hadi kufikia vifo 20,258.

Pia ilielezwa kuwa mapigano yalipamba moto juzi huko kaskazini mwa Ukanda wa Gaza, ambao wanajeshi wa Israel wanatafuta kuudhibiti ili kujikita zaidi upande wa kusini, na moshi mkubwa ulitanda kwenye mji wa Jabaliya, ambao pia ni makazi ya kambi kubwa zaidi ya wakimbizi katika eneo hilo.

Wakazi waliripoti kuendelea kwa mashambulizi ya angani na moto na nchi kavu kwa kutumia vifaru, ambavyo walisema viliingia katika mji huo.

Tawi la kijeshi la Hamas linadai kuharibu vifaru vitano vya Israel, na kuua na kuwajeruhi madereva wa vifaru hivyo, baada ya kutumia tena makombora mawili yaliyorushwa awali na Israel na ambayo hayakulipuka.

Hata hivyo, Wizara ya Afya ya Hamas ilitangaza kuwa Jumamosi makumi ya Wapalestina waliuawa, ikiwa ni pamoja na baadhi ya wauaji wiki hii mitaani wakati wa operesheni ya jeshi la Israel katika eneo la Jabaliya kaskazini mwa Hamas.

"Uvamizi huo ulifanya mauaji kadhaa ya kinyama na kusababisha vifo vya makumi ya mashahidi katika kambi ya Jabaliya, katika eneo la Tal Al-Zaatar na mji wa Jabaliya. Pia waliwanyonga raia kadhaa mitaani," alisema msemaji wa Wizara ya Afya ya Hamas Ashraf al-Qidreh.

"Kiwango cha uharibifu ambacho kimekumba eneo la Tal Al-Zaatar na shule katika kambi ya Jabaliya, ambayo inahifadhi maelfu ya watu waliokimbia makazi yao, ni kubwa na ya kuhuzunisha. Makumi ya mashahidi wamepatikana. Israeli, imewanyonga baadhi yao mbele ya familia zao," serikali ya Hamas ilisema katika taarifa.

Licha ya madai hiyo, ilielezwa kuwa hadi jana Jeshi la Israel halijajibu tuhuma za mauaji yanaodaiwa kutekelezwa na wanajeshi wake.

Lilibainisha kwamba mashambulizi yake dhidi ya malengo ya kijeshi yanazingatia masharti ya sheria ya kimataifa na yanafanywa baada ya tathmini kwamba uharibifu wa ajali unaotarajiwa kwa raia na vitu vya kiraia sio kupita kiasi kuhusiana na faida ya kijeshi inayotarajiwa kutokana na shambulio hilo.

**RFI, BBC**

# ‘WASHINDI TWENDE ZETU IVORY COAST KI-VIP’ WAZOA ZAWADI

Mwandishi Wetu

Abdul Aziz wa Mtwara na Ally Rashidi wa Tanga, wameendeleza ushindi katika droo ndogo ya Kampeni ya ‘Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP’.

Kampeni hiyo inayolenga kuwapeleka nchini Ivory Coast watu sita kushuhudia mubashara fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023 inaendelea kote nchini ikiratibiwa na Kampuni ya Kubashiri ya Betika kwa kushirikiana na Tigopesa.

Droo kubwa ya kutangazwa washindi sita itafanyika Januari 2, na watakaopata tiketi hiyo watasafari kwa gharama za Kampuni ya Betika kwenda Ivory Coast kushuhudia fainali hizo zitakazoanza Januari 13 hadi Februari 11, mwakani.

Washindi hao wataishuhudia mubashara pia timu ya Tanzania (Taifa Stars) ambayo kwenye fainali hizo itacheza mechi yake ya kwanza Januari 17 dhidi ya Morocco, kisha itamalizana na Zambia na DR Congo katika hatua ya makundi.

Kabla ya droo kubwa ya Januari 2, Betika na Tigopesa wamekuwa wakitoa zawadi mbalimbali kwa washindi wanaoendelea kubashiri na Betika wakitumia Tigopesa.

Abdul Aziz na Ally Rashidi ndiyo wameibuka washindi katika droo ndogo ya wiki ya pili na kila mmoja amezawadiwa runinga ya nchi 70, dishi na dekoda yenye kifurushi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa mmoja wa washindi hao, Meneja mauzo wa Tigo Tanzania mkoa wa Tanga, Amani Sailoja, alisema bado fursa za kushinda pesa taslimu kila siku na runinga nyingine kila wiki ipo.

“Unapoendelea kubashiri na Betika kupitia akaunti ya Tigopesa ndipo unajiweka kwenye nafasi kubwa ya kushinda zawadi mbalimbali na kuingia kwenye droo ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP,” alisema Sailoja.

Ally Rashidi, mshindi kutoka Tanga alisema matamanio yake ni kwenda Ivory Coast kushuhudia AFCON.

“Nashukuru nimeshinda runinga, nimekuwa na mwanzo mzuri, nitaendelea kucheza zaidi na zaidi hadi kwenye droo kubwa kwani lengo langu ni kwenda Ivory Coast,” alisema.

Balozi wa Betika mkoani Tanga, Mussa Chausa, alisema ni rahisi kupata nafasi ya kwenda Ivory Coast kushuhudia mubashara Afcon.

“Unachotakiwa ni kuweka pesa kwenye Tigopesa yako na kubeti na Betika,” alisema na kuongeza.

“Pia zawadi nyingine za kila siku na kila wiki za pesa taslimu na runinga, inaendelea hadi Januari 2, mwakani itakapofanyika droo ya washindi sita watakaokwenda Ivory Coast kwenye Afcon.

Wiki ya kwanza washindi wawili kutoka Dodoma walishinda zawadi za wiki na kwa mujibu wa Betika, wote wanaoendelea kubashiri bila kujali wameshinda zawadi za siku au wiki wanaendelea kuingia kwenye kinyang’anyiro cha droo kubwa ya kwenda Ivory Coast.

Stars itashiriki Afcon kwa mara ya tatu msimu huu, baada ya ile ya 1980 nchini Nigeria na 2019 nchini Misri.

Msimu huu Stars ilifuzu baada ya sare ya bila kufungana na wenyeji, Algeria katika mchezo wa mwisho wa Kundi F na kumaliza kundi hilo ikiwa na pointi nane, nyuma ya vinara, Algeria wenye pointi 16 na wote kufuzu wakizipiku Uganda iliyomaliza na pointi saba na Niger pointi mbili.




Mshindi wa ‘Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP’, Ally Rashidi, akiwa ameshika runinga aliyoshinda katika droo ya wiki. Kulia ni Meneja Mauzo wa Mkoa wa Tanga wa Kampuni ya Tigo, Amani Sailoja na kushoto ni Balozi wa Betika Mkoa wa Tanga, Mussa Chausa. **MPIGAPICHA WETU**

# Kipre Junior kinara wa ‘assist’ Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

WAKATI kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki akifikisha bao la 10 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara alilolifunga juzi Uwanja wa Jamhuri Dodoma dhidi ya Tabora United, mchezaji Kipre Junior wa Azam FC, anaongoza kwa kutoa pasi nyingi za mabao mpaka sasa.

Kwa mujibu wa Dawati la Takwimu la Nipashe, Kipre raia Ivory Coast, amefikisha ‘assist’ sita hadi kufikia raundi ya 14 ya Ligi Kuu Tanzania Bara. Mchezaji huyo ambaye hucheza nafasi ya winga na wakati mwingine kiungo mshambuliaji, anafuatiwa na raia mwenzake wa Ivory Coast, Yao Kouassi wa Yanga ambaye mpaka sasa ametoa pasi tano zilizozaa mabao.

Yao, anayecheza nafasi ya beki wa kulia, ndiye anayeongoza kwa ‘assist’ nyingi mpaka sasa kwa upande wa walinzi.

Kiungo mshambuliaji mwingine wa Azam, Feisal Salum ‘Fei Toto’, anaongoza wachezaji wanaoshika nafasi ya tatu kwa ‘assist’ nyingi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Fei Toto ambaye amejiunga na Azam msimu huu akitokea Yanga, ana ‘assist’ nne pamoja na Awesu Awesu wa KMC, Impiri Mbombo wa Tabora United na Lusajo Mwaikenda wa Azam FC.

Wakati raia wa Burkina Faso, Aziz Ki akiwa amefikisha mabao 10 mpaka sasa, Jean Baleke wa Simba na Fei Toto wa Azam wana mabao manane kila mmoja.

Takwimu zinaonesha kuwa nafasi ya tatu ya mabao mengi kwenye orodha ya wafungaji inashikiliwa na Maxi Nzengeli wa Yanga na Waziri Junior wa KMC ambaye juzi alifunga mabao yote mawili kwa timu yake ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba, wakiwa na mabao saba kila mmoja.

Mzimbabwe, Prince Dube wa Azam FC ana mabao sita, huku Adam Adam wa Mashujaa FC na Marouf Tchakei wa Singida Fountain Gate wakiwa na mabao matano kila mmoja.

# Uhamiaji FC kusajili wa5 dirisha dogo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WALINZI wa Mipakani, Uhamiaji FC, watarajia kushusha wachezaji watano katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili na uhamisho wa wachezaji.

Kati ya wachezaji hao watakaowasajili, pia wanatarajia kusajili mchezaji mmoja raia wa Zambia ambaye anakipiga katika moja ya klabu inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Uhamiaji FC, Mwinyi Hamad, alisema mpaka sasa tayari washamalizana na mchezaji mmoja kutoka timu ya Raskazone FC ya Unguja ambayo inacheza Ligi Daraja la Kwanza.

Alisema wanaendelea na mazungumzo na wachezaji wanne ambapo wawili watatoka Tanzania Bara na kwamba hadi mwisho wa mwezi huu watawaweka wazi wachezaji hao baada ya kumalizana nao.

Hamad alisema nafasi wanazozipa kipaumbele katika timu hiyo ni viuongo na washambuliaji, idara ambazo hazikufanya vizuri katika mzunguko kwanza hivyo kuchangia timu hiyo kupata sare nyingi.

Aidha, alisema usajili watakaoufanya utakwenda sambamba na mahitaji ya timu hiyo katika mbio zao za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

“Tunataka kusajili wachezaji ambao wataenda kuongeza nguvu katika safu ya ushambuliaji ambapo hatuko vizuri lengo ni kuimarisha eneo hilo ili kupata matokeo ya alama tatu,” alisema.

Ofisa habari huyo, alisema timu hiyo itakapokamilisha taratibu zake za usajili pia inatarajia kuwapeleka kwa mkopo wachezaji wake wanne katika Klabu za Ligi Kuu Zanzibar na Kanda ili kuongeza viwango vyao vya uchezaji na itawarejesha msimu ujao.

Alisema timu hiyo bado inaendelea na mpango wake wa kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu, hivyo mzunguko wa pili watarudi uwanjani wakiwa bora zaidi.

Uhamiaji FC ipo nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 19 baada ya kushinda michezo mitatu, sare 10 na imefungwa michezo miwili.

## ZISIKUPITE

**PALHINHA MILIONI 60**
KLABU ya Fulham itadai ada ya hadi pauni milioni 60 Januari kwa ajili ya kiungo wa kati wa Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28, ambaye amekuwa akihusishwa na Bayern Munich, Liverpool na Arsenal. ***(Football Insider)***

**TONEY ANUKIA ARSENAL**
ARSENAL wamewasiliana na wawakilishi wa Ivan Toney wanapofikiria kutoa ofa thabiti kwa Brentford kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 27. (***Rudy Galetti***)

**MBAPPE AIGANDA PSG**
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe, hataki kuondoka Paris St-Germain Januari licha ya kwamba mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, utakamilika mwishoni mwa msimu. (***L'Equipe***)

**BERALDO KUTUA LIVERPOOL**
KLABU ya PSG ina makubaliano ya mdomo kumsajili Lucas Beraldo anayelengwa na Liverpool, huku mlinzi huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 20, akitarajiwa kuondoka Sao Paulo kwa pauni milioni 17 Januari. (***Fabrizio Romano via Goal***)

**BUCHANAN ATAJWA INTER**
KLABU ya Inter Milan ina matumaini ya kuipiku Manchester City katika kuinasa saini ya mshambuliaji wa Canada, Tajon Buchanan mwenye umri wa miaka 24. (***Gazzetta dello Sport***)

**BARCO ANG'ARA SOKONI**
KLABU ya Strasbourg inafikiria kumnunua mlinzi wa kushoto wa Boca Juniors na Argentina mwenye umri wa miaka 19, Valentin Barco, ambaye pia analengwa na Chelsea Januari. (***Evening Standard***)

**MAIA AONGEZWA ARSENAL**
ARSENAL imemuongeza kiungo wa kati wa Sao Paulo, Pablo Maia mwenye umri wa miaka 21, kwenye orodha ya wachezaji inaotarajia kuwawinda Januari. (***Football transfers***)

**TOTTENHAM NA DRAGUSIN**
KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia Radu Dragusin baada ya kutuma maskauti kumtazama mlinzi huyo wa Romania mwenye umri wa miaka 21, akiichezea Genoa dhidi ya Juventus wiki iliyopita. ***(Fabrizio Romano)***

**ILING JUNIOR AGOMBEWA**
KLABU ya Aston Villa imeungana na Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kumsajili winga wa Juventus, Samuel Iling-Junior mwenye umri wa miaka 20, kwa dau la takribani pauni milioni 17 huenda likatosha kumnasa mchezaji huyo wa kimataifa wa England. (***Football Insider)***

**FELIX KUBAKISHWA BARCA**
KLABU ya Barcelona ina nia ya kumbakisha mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix, 24. ***(Goal)***

**TAH AWANIWA WEST HAM**
KLABU ya West Ham imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua beki wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 27, ambaye anapendelea kuhamia Ligi Kuu England kuliko Bayern Munich. ***(Bild)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG ACHARUKA UTD KUKUBALI KIPIGO

**LONDON,** England

Ni baada ya West Ham kuifumua mabao mawili, asema hawawezi kujihurumia wenyewe...

ERIK ten Hag amesisitiza Manchester United "haiwezi kujihurumia" baada ya kufungwa mabao 2-0 na West Ham, Jumamosi.

Mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Jarrod Bowen na Mohammed Kudus, yaliwafanya Man United kuwa na mwanzo mbaya zaidi wa msimu tangu mwaka 1930, na kupoteza mechi 13 katika michuano yote kwenye hatua hii ya msimu kwa mara ya pili pekee katika historia yao.

United hawakucheza vizuri katika Uwanja wa London licha ya kutawala mpira kwa muda mrefu na wanatakiwa kujipanga upya kwa haraka dhidi ya Aston Villa kwenye mchezo wa kesho Jumanne pale Uwanja wa Old Trafford.

Ten Hag alisema: "Tunapaswa kucheza mechi mbili zaidi wiki hii lakini hatuwezi kujihurumia.

**"Tunapaswa kuchukua ju kumu, ikiwa wewe ni mchezaji wa Manchester United lazima tufanye hivyo pamoja. Kila mtu anapaswa kuwajibika."**

United wamefunga mabao 18 pekee katika mechi 18 za ligi msimu huu huku Rasmus Hojlund akiwa na wakati mgumu akigusa mpira mara 17 pekee kabla ya kubadilishwa dakika ya 57.

Mbadala wake Marcus Rashford alifanya vema kidogo, kwani Alejandro Garnacho, Antony na Bruno Fernandes wote pia walishindwa kuzifumania nyavu.

"Wana uwezo wa kufanya hivyo," alisema Ten Hag.

"Najua Rashford anaweza kufunga bao. Antony anaweza kufunga, Garnacho anaweza kufunga bao, Bruno anaweza kufunga, Scott McTominay anaweza kufunga bao.

"Tuna uwezo wa kufunga kwenye kikosi chetu na pia kwa kucheza kwa seti, kwa wakati huu hatufanyi hivyo, lazima tushikamane, lakini pia wajiamini kuwa wanaweza kufanya hivyo, wanaweza kufika wapi."

# OSIMHEN AONGEZA MKATABA NAPOLI



**NAPLES,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Napoli, Victor Osimhen, ametia saini mkataba wa nyongeza na sasa atakuwa na mabingwa hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, hadi 2026.

Rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, alichapisha picha zake na Osimhen wakitabasamu na kutia saini makaratasi na kupeana mikono, pamoja na neno "nimekamilika."

Klabu hiyo iliweka picha sawa dakika nne baadaye na nukuu "Victor na Napoli wakiwa pamoja hadi 2026."

Ni habari njema zaidi kwa mchezaji huyo bora wa mwaka wa Afrika.

Mkataba wake ulikuwa unaisha mwaka 2025, na vyombo vya habari vya Italia vimeripoti kuwa mshahara wake umeongezeka zaidi ya mara mbili hadi euro milioni 10 kwa msimu, na kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kati ya euro milioni 120.

Napoli iliripotiwa kukataa ofa ya zaidi ya euro milioni 200 kwa Osimhen kutoka kwa timu ya Saudi Arabia msimu uliopita wa majira ya joto.

Osimhen, ambaye Ijumaa wiki hii anatimiza umri wa miaka 25, alisajiliwa kutoka Lille mwaka 2020 kwa ada ya karibu euro milioni 75 na mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria amejitambulisha kama mmoja wa washambuliaji wa kusisimua zaidi duniani.

Aliisaidia Napoli kutwaa ubingwa wa Serie A msimu uliopita, mabao yake 26 yalitosha kumfanya kuwa mchezaji wa kwanza wa Kiafrika kumaliza kama mfungaji bora wa Ligi Kuu Italia.

Osimhen amekuwa na mwanzo mzuri msimu huu baada ya Rudi Garcia kuchukua nafasi ya kocha aliyeshinda taji, Luciano Spalletti.

# Klopp alilia penalti Liverpool



**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp alimkosoa ofisa wa VAR, David Coote, baada ya Liverpool kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Arsenal kwenye Uwanja wa Anfield, akisema "mtu aliye ofisini" alipaswa kutoa penalti baada ya Martin Odegaard kuuchezea mpira kwa mkono kipindi cha kwanza.

Arsenal ilijihakikisha kuwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England siku ya Krismasi kwa sare hiyo, licha ya Mohamed Salah kufuta bao la kwanza la Gabriel la dakika ya nne, na Liverpool inabakia nafasi ya pili, pointi moja nyuma ya 'Washikabunduki' hao.

Lakini kocha wa Liverpool, Klopp alisema timu yake ilipaswa kupata penalti dakika ya 19 baada ya Odegaard kuonekana kumzuia Salah kuelekea kwenye mpira kwa kuushika mpira eneo la 18.

Mwamuzi Chris Kavanagh aliruhusu mchezo uendelee na haukusimamishwa kwa ukaguzi wa VAR, huku Coote akiamua kuwa Odegaard aliumiliki mpira wakati akianguka.

"Ndio nimeiona," alisema Klopp. "Nina uhakika kuna mtu atakuja kunieleza kwa nini haikuwa mpira wa mkono, lakini sijui ilikuwaje?

"Sisemi kwamba mwamuzi anaweza kuiona kwa sababu sijui alikuwa wapi wakati huo.

"Lakini ni jinsi gani mtu katika ofisi anaweza kuona hilo na asifikie hitimisho kwamba labda inaweza kuwa na thamani ya mwamuzi kuwa na sura nyingine?"

Alipoulizwa kuhusu tukio hilo, kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alisema: "Kulikuwa na maamuzi mawili makubwa, bado sijayaangalia tena. Niliulizwa kabla lakini sijayaona tena."

## Arsenal yaikataa Super League

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema ni muhimu kuwakumbatia mashabiki huku klabu yake ikikataa kushiriki katika pendekezo lililorekebishwa la European Super League (ESL).

Arsenal walikuwa miongoni mwa klabu 12 zilizoungana na mpango wa awali wa ESL mwaka 2021.

Alhamisi mahakama ya Ulaya ya haki ilipiga marufuku klabu kujiunga na ESL kwa kuwa ni kinyume cha sheria, lakini ligi iliyorekebishwa ilipendekezwa saa chache baadaye.

"Wafuasi wa mpira wa miguu na shauku wanayoleta kwenye michezo ndio sababu mchezo huu ni wao," alisema Arteta.

"Maoni yao ni muhimu sana na lazima tuwatunze," aliongeza.

Mwaka wa 2021, timu 12 zilijitenga na kukataa kujisajili na ESL iliyoundwa kushindana na mashindano ya Uefa, lakini mradi huo ulikosolewa na mashabiki, vikundi vya mashabiki, ligi za ndani za Ulaya na hata serikali na kusababisha kuanguka kwa pendekezo hilo ndani ya saa 72.

Miongoni mwa klabu 12 ni Real Madrid na Barcelona pekee ndio waliokubaliana na ligi iliyopendekezwa.

Arsenal wameungana na Chelsea, Tottenham Hotspur, Manchester City na Manchester United katika kutangaza kwamba msimamo wao haujabadilika juu ya ESL na kuthibitisha kujitolea kwao kwa mashindano ya UEFA.

"Tunabaki katika nafasi ileile na tunapenda kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na tutaendelea kufanya hivyo," alisema Arteta.

"Mazungumzo (na wamiliki) tuliyokuwa nayo yalikuwa wazi baada ya yale yaliyotokea miaka miwili iliyopita. Nadhani klabu imetoa tamko ambalo ni wazi na lina uwazi. Tutasimamia hilo."

Pendekezo jipya ni mfumo wa ligi ambao ungejumuisha timu 64 za wanaume na timu 32 za wanawake na uwezo wa kila mwaka wa kupanda na kushushwa daraja.



## HABARI MICHEZO

# BAYPORT YANOGESHA ROMBO MARATHON

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

TAASISI ya Kifedha ya Bayport, imenogesha na kufanikisha mbio za Rombo Marathon 2023, zilizofanyika mjini Rombo, Kilimanjaro jana, zikiwa na lengo la kuhamasisha vivutio vya utalii wilayani humo.

Ikiwa ni mwaka wa pili sasa Rombo Marathon imefanyika ikihudhuriwa na viongozi wa kiserikali, wageni na watu mashuhuri, mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Doto Biteko.

Akizungumza wakati wa mbio hizo, Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Bayport, Nderingo Materu, alisema walikubali kuwa mdhamini wa Rombo Marathon ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali pamoja na mwasisi wa mbio hizo, Waziri wa Elimu na Mbunge wa Rombo, Prof. Adolf Mkenda, katika kukuza utalii pamoja na suala zima la uhifadhi wa mazingira.

"Kama mnavyofahamu sisi Bayport tumekuwa namba moja katika suala la utunzaji wa mazingira kwa njia ya upandaji miti, leo hii tumeamua kudhamini Rombo Marathon na tutaendelea kuunga mkono juhudi zozote nchini zenye lengo la kukuza utalii na kuhifadhi mazingira.

"Lakini kama inavyofahamika umuhimu wa kufanya mazoezi ya mwili kwa ajili ya ubora wa afya za wafanyakazi na familia zetu, tunaamini mbio hizi zitaleta hamasa pia kwa Watanzania kutilia mkazo umuhimu wa kufanya mazoezi ili kujiepusha na magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema Bwana Materu.

Katika hotuba yake, Naibu Waziri Mkuu, Dk. Biteko, alitoa pongezi kwa waandaaji na wadhamini wa mbio za Rombo Marathon, akisema zimekuwa na mafanikio makubwa, lakini kikubwa ikiwa ni kujifunza utamaduni wa Wanarombo pamoja na vivutio vya utalii vinavyopatikana katika wilaya na mkoa huo.

"Natoa pongezi nyingi kwa mwasisi wa Rombo Marathon, Waziri wa Elimu na Mbunge wa Rombo, Prof. Mkenda, natoa pongezi kwa Serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Rombo bila kuwasahau wadhamini wote waliojitolea rasilimali zao kufanikisha tukio hili. "Serikali chini ya Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, itaendelea kuunga mkono juhudi yoyote inayofanywa yenye lengo la kuwaletea maendeleo watu wa Rombo na Watanzania kwa ujumla," alisema Dk. Biteko.

Naye Waziri wa Elimu, Mbunge wa Rombo na muasisi wa mbio hizo, Prof. Mkenda, alimshukuru Dk. Biteko kwa kukubali kuwa mgeni rasmi pamoja na wadhamini wa mbio hizo Taasisi ya Kifedha ya Bayport kwa kufanikisha tukio hilo muhimu kwa maendeleo ya watu wa Rombo na wananchi wa Kilimanjaro.

Mbio za Rombo Marathon zinazofanyika kwa mwaka wa pili sasa, zimeshirikisha mbio za Km. 21, Km 10 na mbio za kujifurahisha za kilomita tano.



Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Taasisi ya Kifedha ya Bayport, Nderingo Materu (wa pili kushoto), Mkuu wa Mauzo wa kampuni hiyo, Lugano Kasambala (kushoto kwake), pamoja na wakimbiaji wengine, wakishiriki mbio za Rombo Marathon 2023 zilizofanyika mjini Rombo, Kilimanjaro jana. Mbio hizo zilizodhaminiwa na Bayport, zina lengo la kuhamasisha vivutio vya utalii mkoani humo. **MPIGAPICHA WETU**

# Zugo azidi kupaa, amshusha Class

**Na Saada Akida**

BONDIA wa Ngumi za Kulipwa nchini, Abeid Zugo, ameweka rekodi mpya kwa kufanikiwa kufikisha hadhi ya nyota nne ya viwango huku akimshusha Tony Rashid na Ibrahim Class katika nafasi za ubora (P4P) wa mabondia wote wa Tanzania kwenye mchezo wa ngumi za kulipwa.

Zugo ambaye amepanda kwa nafasi tano kutoka katika nafasi ya sita ya P4P kwa kumshusha Tony Rashid kutoka ABA Team aliyekuwa katika nafasi ya pili kwenda ya tatu huku Ibrahim Class akitoka nafasi ya tatu hadi ya nne katika viwango hivyo.

Zugo amepanda kwenye nafasi hiyo kwa kufikisha nyota hizo kutokana na kumchapa kwa pointi bingwa wa zamani wa Dunia wa IBF, Simpiwe Veytyeka wa Afrika Kusini huku akiweka rekodi ya kuwa bondia wa kwanza Mtanzania kufikisha nyota nne bila ya kupoteza pambano lolote.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa bondia huyo kutoka Kemmon Sports Promotion, Saada Kasonso, alisema kupanda hadhi kwa bondia wake ni mafanikio makubwa kutokana na mipango mikubwa waliojiwekea ndani ya mwaka ujao.

"Kwetu ni jambo kubwa sana kwa sababu tunafanya kazi kwa kufuata malengo yetu ndani ya mchezo husika na ukiangalia bondia amepanda hadi katika nafasi ya pili kwa ubora Tanzania, hivyo tumepanga makubwa kwa mwaka ujao, " alisema Kasonso.

## Gamondi aukubali muziki Tabora Utd

INATOKA UK 24

go mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, aliwazamisha kwa bao la mpira uliokufa.

Kipindi cha kwanza timu hiyo ilionekana 'kukamatwa' na Yanga waliomiliki mpira muda mwingi, lakini kipindi cha pili Tabora United walibadilika na kuwapa wakati mgumu.

Akizungumza jana jijini hapa, Goran alisema timu yake ilikuwa bora zaidi kipindi cha pili na kama washambuliaji wake wangekuwa makini wangeweza kupata hata sare.

"Timu yangu imebadilika sana kulinganisha na michezo ya nyuma iliyocheza..., katika mchezo na Yanga nadhani watu wameona, kipindi cha pili wachezaji walifanya kile nilichowaelekeza na tulicheza vizuri zaidi, hatukustahili kupoteza pointi zote tatu," alisema Goran.

Aidha, alisema yapo mapungufu wanayotakiwa kuyafanyia kazi na kama watafanikiwa katika hilo watakuwa katika nafasi nzuri ya kupata ushindi katika michezo yao ijayo.

Baada ya juzi kucheza mchezo wao wa nyumbani kwenye Uwanja wa Jamhuri, mechi zinazofuata watacheza kwenye uwanja wao wa nyumbani wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora kutokana na Bodi ya Ligi kuufungulia uwanja huo uliokuwa umefungwa kwa kutokidhi vigezo.

## Benchikha ataka...

INATOKA UK 24

wa mafanikio.

"Lazima tukiri kuwa kikosi chetu kinahitaji mabadiliko makubwa mawili, kwanza ni kuongeza wachezaji wenye ubora, uchu na kiu ya mafanikio.

"Pili ni wachezaji waliopo kuongeze ubora wao wa upambanaji. Huwezi kufanikiwa kwa kuwa na matokeo ya panda shuka, timu kubwa yenye malengo ya ubingwa lazima iwe na mwendelezo wa kupata matokeo mazuri," alisema Ahmed.

Aliongeza kuwa wana miezi miwili ya kufanya mabadiliko hayo mawili makuu ambayo ameona ni tatizo ambalo linawakwamisha mpaka sasa.

Hata hivyo, taarifa zilizolifikia gazeti hili ni kwamba, majina yanayotajwa kuwamo mezani mwa uongozi wa klabu hiyo ni Alves Ngakosso Oko, Hardest Malonga, Moise Gbai, Mohammad Alzabbad, Abdoulaye Djire, Abdul Aziz Issah, Derrick Fordjour, Ibrahim Seck na Jonathan Alukwu.

Michezo
Nipashe Jumatatu Desemba 25, 2023



Ten Hag acharuka United UK. 21




# Gamondi aukubali muziki Tabora Utd

Sasa aonya si mechi zote watashinda mabao mengi, Goran ashangaa kupoteza, asema...

**Na Faustine Feliciane,**
DODOMA

BAADA ya ushindi wa tabu wa bao 1-0 dhidi ya Tabora United katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma juzi, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema si kila mchezo wanaweza kupata mabao mengi kwa kuwa ligi ni ngumu na kila timu inataka kushinda.

Yanga iliyopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 30, moja nyuma ya vinara Azam FC, ina mabao ya kufunga 31 na sita ya kufungwa katika michezo 11 iliyocheza hadi sasa huku vinara hao mabao wameshashuka dimbani mara 13, wakiwa wamecheka na nyavu mara 35 na kuruhusu 10.

Mchezo uliopita kabla ya kucheza na Tabora United juzi, Yanga ilishinda mabao 4-1 dhidi ya Mtibwa Sugar, jambo ambalo mashabiki wengi wa timu hiyo walikuwa wakitegemea karamu hiyo ya kucheka na nyavu ingeendelea, lakini walishangaa kukutana na mlima mrefu.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema si kila mchezo wanaweza kupata mabao mengi na kwamba kwake kikubwa ni pointi tatu.

"Kila timu inatafuta ushindi, na ligi inavyosonga mbele inazidi kuwa ngumu zaidi... kitu cha muhimu ni kuhakikisha tupata pointi bila kuangalia ni magoli mangapi tumefunga, hatuwezi kusema kila mchezo tutakuwa tunashinda mabao matatu, manne au zaidi, hapana..., ila inapotokea tufanyaje hivyo, ligi ni ngumu sana," alisema Gamondi.

Kocha huyo raia wa Argentina, alisema ushindi wa juzi ulikuwa muhimu sana wakati ligi hiyo ikienda kusimama kwa muda kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi na ile ya Mataifa ya Afrika, AFCON.

"Nilitaka ushindi, niliwaambia wachezaji ligi inaenda kusimama kwa muda, hivyo lazima tumalize kwa ushindi ambao utatupa morali pale michezo itakaporejea, lakini pia kama timu twende mapumziko tukiwa tumetoka kushinda," alisema Gamondi.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Tabora United, Goran Kopunovic, alisema walistahili hata sare kwenye mchezo huo kutokana na soka safi walilolionesha wachezaji wake, lakini kiun-

INAENDELEA UK 23

# Benchikha ataka maboresho makini

**Na Saada Akida**

BAADA ya kukiangalia kikosi cha timu yake, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, ni kama ametoa angalizo kwa viongozi wa klabu hiyo kuwa makini wanapoenda sokoni kipindi cha dirisha dogo la usajili kulingana na aina ya wachezaji aliokuwa nao kwa sasa.

Kauli hiyo imekuja baada ya mchezo wa juzi uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMC FC.

Benchikha alisema ana kazi kubwa ya kufanya ndani ya kikosi chake ili kurudi katika ubora na kuendelea kupata ushindi katika michezo iliyopo mbele yao na kufikia malengo yao.

Alisema walicheza vizuri na kutengeneza nafasi nyingi wakashindwa kuzitumia, lakini pia kulikosekana umakini katika safu yake ya ulinzi.


"Kwa sasa tutaendelea kukisuka kikosi katika michuano ya Mapinduzi pamoja na kufanyia kazi maboresho ya kikosi katika maingizo mapya, naamini tutarejesha makali yetu.

"Tuna kazi kubwa ya kufanya, tunahitaji kurudi katika hali ya kawaida na kupigamia mataji, timu inacheza vizuri, lakini kuna vitu vinakosekana ikiwamo kutumia nafasi tunazotengeneza, hilo ndilo jambo tunapaswa kulimaliza," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa wanaelekea kipindi cha mapumziko ambacho watakuwa makini katika maboresho ya kikosi kulingana na mahitaji ya timu lakini pia kutumia Kombe la Mapinduzi kuandaa kikosi imara.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, pia alikiri timu yao inahitaji mabadiliko makubwa kwa kusajili wachezaji wazuri wenye uchu

INAENDELEA UK 23




GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002